**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

National Development Plan | Strategy and Plans Development Books

2019

# Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa,2019

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/755

*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

# MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2019/20

OKTOBA, 2018

# MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2019/20

3.3 Hatua za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ---------- 13
3.3.1 Miradi Mikubwa ya Kielelezo ---------- 13
3.3.2 Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa msingi wa Uchumi wa Viwanda ---------- 16
3.3.3 Kuhmgamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu ---------- 22
3.3.4 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji ---------- 27
3.3.5 Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango ---------- 32
3.3.5.1 Ufuatiliaji wa Miradi katika Mwaka 2017/18 ---------- 32
3.3.5.2 Changamoto Zilizobainishwa katika Utekelezaji wa Miradi Iliyofuatiliwa ---------- 32
3.3.5.3 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango na Hatua Zilizochukuliwa ---------- 33

SURA YA NNE ---------- 34
MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2019/20 ---------- 34
4.1 Utangulizi ---------- 34
4.2 Misingi na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi ---------- 34
4.2.1 Msingi ya Mpango kwa Mwaka 2019/20 ---------- 34
4.2.2 Shabaha za Ukuaji wa Uchumi ---------- 34
4.3 Miradi Mikubwa ya Kielelezo na Itakayopewa Msukumo wa Kipekee ---------- 35
4.3.1 Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji Rufiji - MW 2,100 ---------- 35
4.3.2 Kuendeleza ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Standard Gauge 35
4.3.3 Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania ---------- 36
4.3.4 Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) ---------- 36
4.3.5 Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia - Lindi ---------- 36
4.3.6 Kiwanda cha Kufua Chuma cha Liganga ---------- 36
4.3.7 Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi ---------- 36
4.3.8 Kusomesha kwa Wingi Wataalam kwenye Fani na Ujuzi Adimu ---------- 37
4.4 Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda 38
4.4.1 Viwanda ---------- 38
4.4.2 Kilimo ---------- 39
4.4.3 Wanyamapori ---------- 40
4.4.4 Madini ---------- 40
4.4.5 Utalii, Biashara na Masoko ---------- 41
4.5 Kufungamanisha Uchumi na Maendeleo ya Watu ---------- 41
4.5.1 Elimu na Ujuzi ---------- 41
4.5.2 Afya na Ustawi wa Jamii ---------- 42
4.5.3 Maji na Usafi wa Mazingira ---------- 43

YALIYOMO


SURA YA KWANZA ---- 1
UTANGULIZI ---- 1
1.1 Umuhimu wa Mapendekezo ya Mpango ---- 1
1.2 Mazingira Yanayoongoza Mpango ---- 1
1.3 Ushirikishwaji wa Wadau ---- 2
1.4 Mpangilio wa Kitabu ---- 2

SURA YA PILI ---- 3
HALI YA UCHUMI ---- 3
2.1. Utangulizi ---- 3
2.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi ---- 3
2.2.1. Uchumi wa Dunia ---- 3
2.2.1.1. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea ---- 3
2.2.1.2. Uchumi wa Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea ---- 3
2.2.2. Uchumi wa Afrika na Kanda ---- 4
2.2.2.1. Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ---- 4
2.2.3. Uchumi wa Taifa ---- 4
2.2.3.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi ---- 4
2.2.3.2 Wastani wa Pato la kila Mtu ---- 5
2.2.3.3 Mwenendo wa Bei Nchini ---- 6
2.2.3.4 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki ---- 7
2.2.3.5 Sekta ya Nje ---- 7
2.2.3.6 Sekta ya Fedha ---- 8
2.2.3.7 Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ---- 9
2.2.3.8 Deni la Serikali ---- 9
2.3 Idadi ya Watu na Mabadiliko ya Maisha ---- 10
2.3.1 Ongezeko la Idadi ya Watu ---- 10
2.3.2 Mwenendo wa Viashiria vya Umaskini ---- 10
2.3.2.1 Umiliki wa Samani/ Mali za Kudumu ---- 11
2.3.2.2 Upatikanaji wa Chakula ---- 11

SURA YA TATU ---- 12
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO ---- 12
3.1 Utangulizi ---- 12
3.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo ---- 12
3.2.1 Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2017/18 ---- 12
3.2.2 Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2018/19 ---- 13

4.5.4 Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ---------- 43
4.5.5 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ---------- 44
4.5.6 Utawala Bora na Huduma Bora kwa Wananchi ---------- 44
4.5.7 Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ---------- 44
4.6 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji ---------- 45
4.6.1 Miundombinu ---------- 45
4.6.2 Ardhi na Maeneo ya Uwekezaji na Biashara ---------- 47
4.6.3 Huduma za Fedha ---------- 47
4.6.4 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa ---------- 47
4.6.5 Ushiriki wa Sekta binafsi, Mashirika na Taasisi za Umma katika Mpango ---------- 47
4.7 Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango ---------- 49

SURA YA TANO ---------- 50
UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2019/20 ---------- 50
5.1 Utangulizi ---------- 50
5.2 Gharama za Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2019/20 ---------- 50
5.3 Vyanzo vya Mapato kwa Mwaka 2019/20 ---------- 50

SURA YA SITA ---------- 52
UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA ---------- 52
6.1 Utangulizi ---------- 52
6.2 Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21 ---------- 52
6.3 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa 2019/20 ---------- 52
6.4 Mgawanyo wa Majukumu ---------- 53

SURA YA SABA ---------- 54
VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA KINGA ---------- 54
7.1 Utangulizi ---------- 54
7.2 Vihatarishi vya Ndani na Mikakati ya Kukabiliana navyo ---------- 54
7.3 Vihatarishi vya Nje na Mikakati ya Kukabiliana navyo ---------- 55

Kiambatisho I: Ratiba ya Maandalizi ya Mpango 2019/20 ---------- 57

Kiambatisho II: Miradi Iliyofuatiliwa katika Mwaka 2017/18 ---------- 59

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Umuhimu wa Mapendekezo ya Mpango

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 yanalenga kuweka msingi kwa ajili ya maandalizi ya Mpango wa Mwaka 2019/20. Mpango huo utakuwa wa nne katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21, wenye dhima ya Kujenga Uchumi wa Viwanda ili Kuchochea Mageuzi ya Uchumi na Maendeleo ya Watu. Mpango huo utajikita katika kutekeleza maeneo manne ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Miaka Mitano, ambayo ni:- (i) Viwanda vya kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda; (ii) Kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu; (iii) Uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji; na (iv) Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango. Wizara za kisekta na taasisi za umma zinapaswa kuzingatia maeneo haya ya kipaumbele katika maandalizi ya mipango na bajeti kama inavyoelekezwa katika Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2019/20 – 2021/22.

### 1.2 Mazingira Yanayoongoza Mpango

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/20 yamejikita katika kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano hususan kwa miradi ambayo utekelezaji wake unaendelea. Katika kuhakikisha kuwa malengo husika yanafikiwa, Serikali imeandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Mkakati huu unatoa mwongozo kuhusu utekelezaji, ugharamiaji, ufuatiliaji na tathmini, na mawasiliano na wadau wa Mpango.

Mapendekezo ya Mpango yamejumuisha miradi mbalimbali ya kimkakati ikijumuisha: Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania; Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge;* Kusomesha Kwa Wingi Katika Fani Na Ujuzi Adimu Na Maalum; Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi; Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi; na Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji Rufiji - MW 2,100.

Vile vile, Mapendekezo yamezingatia maeneo manne ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Katika eneo la ukuzaji uchumi msisitizo umewekwa katika viwanda vya uzalishaji wa bidhaa kwa kutumia malighafi kutoka nchini (pamba hadi nguo, ngozi na bidhaa za

ngozi, madawa na vifaa tiba), Kilimo, Maliasili na Utalii, Madini, Biashara na Uwekezaji. Katika eneo la maendeleo ya watu msisititizo umewekwa katika Mabadiliko ya hali ya hewa na tabia nchi, Elimu, Afya, Maji, Utawala Bora na Ulinzi na Usalama. Katika eneo la kuboresha mazingira ya kufanya biashara msisitizo umewekwa katika miundombinu ya usafirishaji; ukuaji wa miji na majiji; Nishati; na Sayansi, Teknologia na Ubunifu. Katika eneo la kuimarisha utekelezaji wa mpango msisitizo umewekwa katika kuboresha Ufuatiliaji na Tathmini; kuimarisha uandaaji wa miradi; na kuimarisa upatikanaji na usimamizi wa rasilimali.

Aidha, Mapendekezo ya Mpango yamezingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21); Sera na Mikakati mbalimbali ya kisekta, Kikanda (EAC na SADC) na Umoja wa Afrika; Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Agenda 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu.

## 1.3 Ushirikishwaji wa Wadau

Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango yameshirikisha wadau mbalimbali ikijumuisha Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi. Aidha, washirika wa maendeleo wameshirikishwa kupitia majadiliano ya kufikia maeneo ya ushirikiano, ufadhili wa miradi mahsusi na misaada ya kisekta.

## 1.4 Mpangilio wa Kitabu

Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango kimegawanyika katika sura saba (7): Sura ya kwanza ni utangulizi; Sura ya pili inaainisha mapitio ya hali ya uchumi; Sura ya tatu inahusu utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2017/18 na robo ya kwanza ya mwaka 2018/19; Sura ya nne inaainisha maeneo ya kipaumbele kwa 2019/20; Sura ya tano inaeleza ugharamiaji wa Mpango; Sura ya sita inaainisha mfumo na utaratibu wa ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa za utekelezaji wa Mpango; na Sura ya saba inabainisha vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na hatua za kukabiliana navyo.

# SURA YA PILI

# HALI YA UCHUMI

## 2.1. Utangulizi

Mapitio ya hali ya uchumi ni muhimu katika kuainisha na kutathmini mafanikio na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa mipango na mikakati ya maendeleo katika kipindi husika. Katika kufanikisha hili, uchambuzi wa kina wa viashiria vya hali ya uchumi kwa kutumia takwimu katika kila hatua ya maandalizi na utekelezaji wa mipango ni mojawapo ya hitaji muhimu. Hivyo, sura hii inawasilisha uchambuzi wa baadhi ya viashiria vya uchumi jumla kwa mwaka 2018 kwa kutumia vigezo mbalimbali.

## 2.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi

### 2.2.1. Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Julai 2018, Uchumi wa dunia kwa mwaka 2018 unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.9 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2017. Ukuaji huu utatokana na kuendelea kuimarika kwa uwekezaji na biashara kimataifa, ukuaji imara miongoni mwa nchi zinazoibukia za Asia na kuimarika kwa bei za mauzo miongoni mwa nchi zinazouza zaidi nje.

#### 2.2.1.1. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea

Uchumi kwa nchi zilizoendelea unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 2.4 mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2017. Ukuaji huu utatokana na hatua za kukuza mitaji na uwekezaji na sera za kuongeza ukwasi miongoni mwa nchi zilizoendelea.

#### 2.2.1.2 Uchumi wa Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea

Uchumi kwa nchi zinazoibukia na zinazoendelea unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2017. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji mwaka 2018 kutatokana na matarajio ya kuongezeka kwa uwekezaji na uzalishaji katika nchi ya India na baadhi ya nchi za Asia (Indonesia, Malaysia, Ufilipino, Singapore, na Thailand). Jedwali Na. 2.1 linaonesha mwenendo wa ukuaji wa Pato la Dunia kuanzia mwaka 2015 hadi 2017 na matarajio kwa mwaka 2018 na 2019.

**Jedwali 2.1: Ukuaji wa Pato halisi la Dunia 2015 - 2017, na Matarajio 2018 – 2019**

| Kundi/Mwaka | Ukuaji Halisi (asilimia) | | | Matarajio (asilimia) | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 |
| Dunia | 3.1 | 3.2 | 3.7 | 3.9 | 3.9 |
| Nchi Zilizoendelea | 2.1 | 1.7 | 2.3 | 2.4 | 2.2 |
| Nchi Zinazoibukia na Zinazoendelea | 4.3 | 4.3 | 4.7 | 4.9 | 5.1 |
| Nchi Zinazoibukia Barani Asia | 6.8 | 6.4 | 6.5 | 6.5 | 6.5 |
| Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara | 3.4 | 1.3 | 2.8 | 3.4 | 3.8 |

**Chanzo**: Shirika la Fedha la Kimataifa, Julai, 2018

### 2.2.2 Uchumi wa Afrika na Kanda

Kwa upande wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, uchumi unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.8 mwaka 2017. Ukuaji huu utachangiwa na kuongezeka kwa shughuli za uchimbaji madini na uzalishaji wa mazao ya kilimo na bidhaa za viwandani.

#### 2.2.2.1. Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, uchumi unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2018 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2017. Ukuaji huo utatokana na kuendelea kuimarika kwa hali ya hewa, upatikanaji wa chakula na kuendelea kutekelezwa kwa miradi mbalimbali ya maendeleo. Jedwali Na. 2.2 linaonesha mwenendo wa ukuaji halisi na matarajio ya Pato la Taifa kwa Nchi za Afrika Mashariki kuanzia mwaka 2015 hadi 2019.

**Jedwali 2.2: Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa kwa Nchi za Afrika Mashariki; 2015 – 2017 na Matarajio ya ukuaji 2018 na 2019**

| Nchi/Ukuaji | Ukuaji Halisi (asilimia) | | | Matarajio ya Ukuaji (asilimia) | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 | 2019 |
| Tanzania | 7.0 | 7.0 | 7.1 | 7.2 | 7.3 |
| Kenya | 5.6 | 6.0 | 4.8 | 5.5 | 6.0 |
| Uganda | 4.8 | 4.9 | 4.5 | 5.2 | 5.8 |
| Rwanda | 6.9 | 6.0 | 6.1 | 7.2 | 7.8 |
| Burundi | -4.0 | -0.5 | - | 0.1 | 0.4 |
| wastani | 4.1 | 4.7 | 4.5 | 5.0 | 5.5 |

**Chanzo:** Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)


### 2.2.3. Uchumi wa Taifa

#### 2.2.3.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

Ofisi ya Taifa ya Takwimu imefanya mapitio ya takwimu za Pato la Taifa kwa kubadili mwaka wa kizio kutoka 2007 kwenda 2015. Hivyo, kwa mujibu wa

takwimu za Pato la Taifa zilizorekebishwa kwa kutumia mwaka wa kizio 2015 (Base year 2015), Pato la Taifa kwa bei za miaka husika lilikuwa shilingi milioni 125,624,406 mwaka 2017 ikilinganishhwa na Shilingi milioni 111,537,022 mwaka 2016. Aidha, Pato la Taifa katika kipindi cha robo ya kwanzo ya mwaka 2018 lilikua kwa asilimia 8.4 ikilinganishwa na asilimia 5.7 kipindi kama hicho mwaka 2017. Shughuli za kiuchumi zilizochangia zaidi ukuaji huu ni ujenzi (asilimia 28.2); kilimo kinachojumuisha mazao, mifugo, misitu na uvuvi (asilimia 23.1); Utawala na Ulinzi (asilimia 7.4); na Usafirishaji na uhifadhi mizigo (asilimia 7.3).[1] Katika kipindi husika, shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kasi kubwa ni pamoja na ujenzi (asilimia 20.0), Habari na mawasiliano (asilimia 18.3), utawala na ulinzi (asilimia 15.5), na Shughuli za Kitaalam, Kisayansi na Kiufundi (asilimia 11.3). Vile vile, sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 7.1. Aidha, shughuli za kiuchumi zenye mchango mkubwa zaidi kwenye Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika ni kilimo (mazao, mifugo, uvuvi na misitu) na ujenzi ambazo zilichangia kwa asilimia 31.4, na 13.9 kwa mtiririko huo.

**Kielelezo Na.2.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Pato Halisi la Taifa katika Kipindi cha Robo Mwaka ya kwanza, 2012 – 2018**




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

### 2.2.3.2 Wastani wa Pato la kila Mtu

Kwa mujibu wa takwimu za Pato la Taifa zilizorekebishwa kwa kutumia mwaka wa kizio 2015 (Base year 2015), Pato la Taifa kwa bei za miaka husika lilikuwa shilingi milioni 125,624,406 mwaka 2017 ikilinganishhwa na Shilingi milioni 111,537,022


[1] Takwimu hizi zinaainisha mchango wa sekta husika katika ukuaji wa uchumi na sio ukuaji wa sekta husika kwa kipindi husika. Vile vile, mchango wa sekta husika katika ukuaji wa uchumi sio sawa na mchango wa sekta katika Pato la Taifa.

mwaka 2016. Aidha, Tanzania bara ilikadiriwa kuwa na watu 51,020,337 mwaka 2017 ikilinganishwa na watu 48,676,698 mwaka 2016. Kwa kutumia takwimu hizo, Pato la wastani la kila mtu kwa mwaka 2017 lilikuwa shilingi 2,462,242 ikilinganishwa na shilingi 2,291,384 mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 7.5. Aidha, Pato la wastani kwa kila mtu katika Dola za Marekani lilio ngezeka hadi kufikia Dola 1,104.7 mwaka 2017 kutoka Dola 1,052.5 mwaka 2016.

**2.2.3.3 Mwenendo wa Bei Nchini**

Hali ya upatikanaji wa chakula ni mojawapo ya kigezo muhimu kinachochangia mabadiliko ya mfumuko wa bei za bidhaa na huduma. Katika kipindi cha Januari hadi Agosti 2018 mwenendo wa mfumuko wa bei umeendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja ambapo kwa mwezi Januari 2018 ulikuwa asilimia 4.0, Juni 2018 asilimia 3.4 na Agosti asilimia 3.3. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Agosti 2018 mwenendo wa bei ulikuwa kama ifuatavyo: mfumuko wa bei za vyakula ulipungua kutoka asilimia 6.7 hadi asilimia 3.2; na mwenendo wa mfumuko wa bei za nishati uliongezeka kutoka asilimia 10.4 hadi asilimia 18.7, mwenendo huu ulichangiwa na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia.

**Kielelezo Na. 2.2: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei (Januari 2017 – Agosti 2018).**



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Wastani wa mfumuko wa bei katika kipindi cha Januari hadi Agosti 2018 ulikuwa asilimia 3.7 ikilinganishwa na asilimia 5.6 kipindi kama hicho mwaka 2017. Vile vile, katika kipindi hicho, mfumuko wa bei za vyakula ulipungua kwa wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 10.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2017.

### 2.2.3.4 Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki

Katika kipindi cha Januari hadi Agosti 2018, mfumuko wa bei katika nchi za ukanda wa Afrika Mashariki umeendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja. Katika kipindi hicho wastani wa mfumuko wa bei kwa Tanzania ulikuwa asilimia 3.7, Uganda asilimia 2.5, Burundi asilimia -0.5, Kenya asilimia 4.2 na Rwanda asilimia 0.2. Utulivu wa mfumuko wa bei katika nchi hizo umetokana na hali nzuri ya hewa iliyochangia kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya chakula cha kutosha katika ukanda huo.

**Jedwali Na. 23: Mfumuko wa Bei katika nchi za Afrika Mashariki, Januari – Agosti 2018**

| Nchi/Mwezi | Mwaka 2018 | | | | | | | | Wastani Jan.-Agosti 2018 | Wastani Jan.-Agosti 2017 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jan | Feb | Mach | Apr | Mei | Jun | Jul | Ago | | |
| Tanzania | 4.0 | 4.1 | 3.9 | 3.8 | 3.6 | 3.4 | 3.3 | 3.3 | 3.7 | 5.7 |
| Kenya | 4.8 | 4.5 | 4.2 | 3.7 | 4.0 | 4.3 | 4.5 | 4.0 | 4.2 | 9.3 |
| Uganda | 3.0 | 2.1 | 2.0 | 1.8 | 1.7 | 2.2 | 3.1 | 3.8 | 2.5 | 6.3 |
| Rwanda | 0.1 | -1.3 | -1.4 | -0.1 | 1.8 | 1.4 | 0.6 | 0.6 | 0.2 | 11.0 |
| Burundi | 6.1 | -1.3 | -2.6 | -1.7 | -1.0 | -0.4 | -0.8 | -2.3 | -0.5 | 17.0 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Taarifa za Nchi Husika.

### 2.2.3.5 Sekta ya Nje

**(a) Urari wa Malipo ya Kawaida**

Katika mwaka 2017/18, urari wa malipo ya kawaida ulikuwa na nakisi ya Dola za Marekani milioni 1,778.0 ikilinganishwa na nakisi ya Dola za Marekani milioni 1,437.8 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la nakisi kwa asilimia 23.7. Hii inatokana na ongezeko la uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi pamoja na malipo nje ya nchi hususan malipo ya riba za mikopo. Katika kipindi husika, mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yalikuwa Dola za Marekani milioni 8,949.40 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 8,701.7 mwaka 2016/17, sawa na ongezeko la asilimia 28. ongezeko hilo lilitokana na ongezeko la thamani ya mauzo ya mazao ya korosho, karafuu, tumbaku, chai na mkonge; pamoja na kuimarika kwa bei za dhahabu katika soko la Dunia. Thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi ilikuwa dola za Marekani milioni 10,157.60 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 9,701.1 mwaka 2016/17 kutokana na ongezeko la uagizaji wa bidhaa za mlaji na malighafi hususan bidhaa za petroli na malighafi za viwandani.

**(b) Akiba ya Fedha za Kigeni**

Katika kipindi cha mwaka unaoishia Juni 2018, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Marekani milioni 5,483.9 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 5,000 4 Juni 2017. Hii ni sawa na uwezo wa kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 5.6 (bila kujumuisha bidhaa za uwekezaji wa moja kwa moja).

**2.2.3.6 Sekta ya Fedha**

(a) **Ujazi wa Fedha na Karadha**

Katika mwaka 2017/18, Serikali iliendelea kutekeleza sera za kuongeza ukwasi katika uchumi ili kuchochea ukuaji wake. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) uliongezeka kwa wastani wa asilimia 7.0 kufikia shilingi bilioni 25,294.5 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 4.5 mwaka 2016/17. Ongezeko hili lilichangiwa na kuimarika kwa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi na rasilimali za kigeni katika benki za biashara.

**(b) Mwenendo wa Sekta ya Benki**

Katika mwaka 2017/18, sekta ya benki iliendelea kuwa imara, salama na yenye kutengeneza faida, ikiwa na mtaji na ukwasi wa kutosha. Katika kipindi hicho, uwiano wa mtaji wa msingi kwa rasilimali za benki ulifikia asilimia 18.2 ukiwa juu ya kiwango cha chini kinachohitajika kisheria cha asilimia 10.0, ingawa ilipungua kidogo ikilinganishwa na asilimia 18.3 iliyofikiwa mwaka 2016/17. Vile vile, uwiano wa rasilimali kwa amana zinazoweza kubadilishwa kwa muda mfupi kuwa fedha taslimu ulifikia asilimia 37.6, na kukidhi kiwango cha chini kinachohitajika kisheria cha asilimia 20, ingawa ni chini kidogo ya asilimia 38.1 iliyofikiwa mwezi Juni 2017.

**(c) Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi**

Mikopo kwa sekta binafsi kwa mwaka 2017/18 iliendelea kuimarika kufuatia utekelezaji wa sera ya kuongeza ukwasi kwenye uchumi pamoja na hatua zilizochukuliwa na benki za biashara kupunguza mikopo chechefu. Kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kukua ambapo hadi kufikia mwezi Juni 2018 ilifikia asilimia 4.0 ikilinganishwa na asilimia 13 mwezi Juni 2017. Sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa katika shughuli binafsi (asilimia 22.8) ikifuatiwa na shughuli za biashara (asilimia 20.5), shughuli za uzalishaji viwandani (asilimia 11.1) na kilimo (asilimia 6.9).

**(d) Mwenendo wa Viwango vya Riba**


Mwaka 2017/18 Serikali iliendelea kutekeleza sera za fedha ili kuongeza ukwasi na utulivu wa riba katika kuchochea ukuaji wa uchumi. Kutokana na utekelezaji wa

sera hizo, riba za dhamana za muda mfupi za Serikali zilipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 5.59 Juni 2018 kutoka wastani wa asilimia 7.64 mwezi Juni 2017. Hata hivyo, riba za mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi zimeendelea kuongezeka na riba za amana zimepungua. Riba za mikopo ziliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 17.83 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 16.61 mwaka 2016/17, ongezeko hilo lilitokana na tahadhari zilizochukuliwa na benki za biashara kudhibiti mikopo chechefu.

**2.2.3.7 Mwenendo wa Thamani ya Shilingi**

Katika mwaka 2017/18, mwenendo wa thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani ulikuwa tulivu kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti. Dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa Shilingi 2,231.17 hadi Shilingi 2,264.97 ikilinganishwa na Shilingi 2,170.4 hadi Shilingi 2,230.1 mwaka 2016/17. Kielelezo Na. 2.3 kinaonesha mwenendo wa thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani kwa kipindi husika.

**Kielelezo Na. 2.3: Mwenendo wa Thamani ya Shilingi Dhidi ya Dola ya Marekani (Wastani wa mwezi husika)**



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

**2.2.3.8 Deni la Serikali**

Hadi Juni 2018, deni la Serikali lilifikia dola za Marekani milioni 23,234.26 sawa na asilimia 39.4 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 21,623.26 Juni 2017. Ongezeko la deni lilitokana na kupokelewa kwa mikopo mipya na mauzo ya dhamana za Serikali kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na bajeti. Deni la Serikali ni himilivu na Serikali inaendelea kuchukua tahadhari muhimu katika kukopa ikijumuisha kukopa kwenye vyanzo vyenye masharti nafuu na

kuelekeza mikopo husika katika miradi ya kimkakati na yenye manufaa makubwa kwa Taifa.

## 2.3 Idadi ya Watu na Mabadiliko ya Maisha

### 2.3.1 Ongezeko la Idadi ya Watu

Kasi ya ongezeko la idadi ya watu nchini imeendelea kuongezeka, japokuwa zipo fursa mbalimbali za kimaendeleo zitokanazo na ongezeko hilo ikiwemo kuongezeka nguvukazi ya kutosha kwa ajili ya ujenzi wa uchumi, ajira na kipato. Kwa upande mwingine, ongezeko hilo linatoa changamoto ya upatikanaji wa ajira huduma za msingi za kijamii kama vile afya, elimu, maji, lishe na nishati.

Kwa mujibu wa taarifa ya makadirio ya idadi ya watu ya Februari 2018, Tanzania Bara ilikadiriwa kuwa na watu 52,619,314 ikijumuisha wanaume 25,741,567 na wanawake 26,877,747. Katika idadi hiyo, watoto wenye umri kati ya miaka 0 -14 ni 22,998,096 (asilimia 43.7), umri kati ya miaka 15 - 64 ambao ndio nguvu kazi ni 27,957,929 (asilimia 53.1) na umri wa miaka 65 na zaidi ni 1,663,289 (asilimia 3.1). Aidha wastani wa ongezeko la idadi ya watu ni asilimia 3.1. Serikali inaendelea na juhudi za kuhakikisha kuwa ongezeko la idadi ya watu linaendana na ongezeko la uzalishaji na ukuzaji tija katika uchumi. Juhudi hizo ni pamoja na kuendelea kuimarisha huduma mbalimbali za jamii zikiwemo; elimu msingi bila ada, mafunzo na huduma za afya, fursa za ajira, upatikanaji wa maji safi, miundombinu ya barabara, nishati pamoja na uboreshaji wa nyumba na makazi.

Vile vile, Taarifa ya makadirio ya idadi ya watu ya Februari 2018 inaonesha kuongezeka kwa umri wa kuishi kwa Tanzania bara kutoka wastani wa miaka 62.2 mwaka 2013 hadi wastani wa miaka 64.9 mwaka 2018 na miaka 65.4 mwaka 2019.

### 2.3.2 Mwenendo wa Viashiria vya Umaskini

Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya uliofanyika mwaka 2012 takwimu zinaonesha kuwa asilimia 28.2 ya wananchi wa Tanzania Bara wapo chini ya mstari wa umaskini wa mahitaji ya msingi ambapo, vijijini ni asilimia 33.3, maeneo mengine ya mijini ni asilimia 21.7 na Dar es salaam ni asilimia 4.2. Vile vile, asilimia 9.2 ya watanzania wapo chini ya mstari wa umaskini wa chakula wakati maeneo ya vijijini ni asilimia 11.3, maeneo mengine ya mijini ni asilimia 8.7 na Dar es salaam ni asilimia 1.0. Lengo la Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21 ni kupunguza umaskini wa mahitaji ya msingi na chakula ni kufikia asilimia 16.7 na 5.7 mwaka 2020 kwa mtiririko huo.

Serikali inaendelea na jitihada za kupambana na umaskini nchini kwa kuboresha huduma za jamii zikiwemo elimu, afya, nishati na maji. Vile vile, Serikali imeendelea kuboresha huduma za mawasiliano na usafirishaji na kuwezesha kuongezeka kwa umiliki wa mali zikijumuisha simu za viganjani, pikipiki na radio.

### 2.3.2.1 Umiliki wa Samani/ Mali za Kudumu

Umiliki wa samani ni moja wapo ya kiashiria cha kutathmini hali ya umaskini katika ngazi ya kaya. Mali za kudumu ni pamoja na simu za mkononi, friji, pikipiki, magari, redio, baiskeli na ardhi. Tafiti mbalimbali zilizofanyika kati ya mwaka 2010 na 2016 zinaonesha kuwa idadi ya kaya zinazomiliki simu za mkononi zimeongezeka kutoka asilimia 45.4 mwaka 2010 hadi asilimia 78.1 mwaka 2016. Pia, idadi ya kaya zinazomiliki runinga, pikipiki, jokofu na magari zimeongezeka kwa kiasi kikubwa kati ya mwaka 2010 na 2016 ikiashiria kuwa kipato cha kaya kimeongezeka. Jedwali Na. 2.4 linaonesha kiwango cha umiliki wa samani/mali za kudumu kati ya mwaka 2010 na mwaka 2016.

**Jedwali Na. 2.4: Umiliki wa Samani/Mali za Kudumu**

| Mwaka | 2010 | 2016 |
|---|---|---|
| Simu za mkononi | 45.4 | 78.1 |
| Runinga | 12.7 | 23.6 |
| Pikipiki | 2.9 | 7.3 |
| Jokofu | 5.5 | 8.3 |
| Magari | 1.8 | 2.1 |
| Redio | 60 | 56.5 |
| Baiskeli | 43.1 | 29.6 |

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

### 2.3.2.2 Upatikanaji wa Chakula

Hali ya uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya chakula nchini kwa kutumia mlinganisho wa nafaka imeendelea kuimarika. Katika msimu wa 2017/18, uzalishaji ulifikia tani milioni 15.9 ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 13.3 ya chakula kwa kipindi hicho. Kutokana na uzalishaji huo, nchi ilikuwa na ziada ya tani milioni 2.6 za mazao yote ya chakula na hivyo, kujitosheleza kwa asilimia 120. Aidha, hadi kufikia Januari, 2018 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula ulikuwa umenunua jumla ya tani 26,038 za mahindi na akiba ya chakula iliyopo ghalani ni tani 92,074.

# SURA YA TATU

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Mwaka 2017/18 na robo ya kwanza ya mwaka 2018/19, kwa kuelezea bajeti iliyopangwa na kiasi cha fedha kilichotumika kwa kipindi husika. Pia inaeleza hatua mbalimbali zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

### 3.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo

#### 3.2.1 Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2017/18

Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 11,432.7 zilitengwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Kiasi hicho kilijumuisha Shilingi bilioni 8,969.75 fedha za ndani na bilioni 3,029.85 fedha za nje. Hadi Juni 2018, Shilingi bilioni 6,543.2 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ikiwa ni asilimia 57 ya lengo. Fedha zilizotolewa zinajumuisha fedha za ndani Shilingi bilioni 5,068.8 na fedha za nje Shilingi bilioni 1,474.4.

Utoaji wa fedha za maendeleo chini ya makadirio uliakisi kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa fedha zinazotokana na misaada pamoja na mikopo ya kibiashara. Hata hivyo, miradi yenye vyanzo vya fedha mahsusi ilipata fedha zote zilizokusanywa katika kipindi husika.

Fedha za maendeleo zilizotolewa zilizingatia miradi iliyopewa kipaumbele katika kipindi hicho ambayo ni pamoja na: ujenzi na ukarabati wa reli Shilingi bilioni 1,222.5; ujenzi na ukarabati wa barabara Shilingi bilioni 1,528.0; usambazaji wa Umeme Shilingi bilioni 723.1; kuboresha Shirika la Ndege Tanzania Shilingi bilioni 238.1; ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere (Terminal III) Shilingi bilioni 169.3; maji mijini na vijijini Shilingi bilioni 150.3; mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu Shilingi bilioni 443.1; ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi Shilingi bilioni 125; ujenzi na ukarabati wa hospitali za wilaya, vituo vya afya na nyumba za watumishi Shilingi bilioni 177.2; utoaji wa elimumsingi bila ada Shilingi bilioni 249.7; ujenzi wa ukuta wenye mzingo wa kilomita 24.5 kuzunguka migodi ya Tanzanite – Mirerani; na kuanza kujenga vituo saba (7) vya umahiri katika maeneo ya Mpanda, Musoma, Chunya, Handeni, Tanga, Bariadi na Songea. Aidha, fedha zilizotolewa na Washirika wa Maendeleo zilielekezwa kwenye miradi ya Barabara, Nishati, Afya, Maji, Elimu na Kilimo.

### 3.2.2 Bajeti ya Maendeleo ya Mwaka 2018/19

Katika mwaka 2018/19, Serikali ilitenga Shilingi bilioni 12,007.3 kugharamia bajeti ya maendeleo, sawa na asilimia 37 ya bajeti ya Serikali. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 9,876.4 ni fedha za ndani, zikijumuisha Shilingi bilioni 345.7 za Halmashauri na Shilingi bilioni 2,130.9 ni fedha za nje. Hadi Agosti 2018, jumla ya Shilingi bilioni 964.0 zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya kugharamia matumizi ya maendeleo. Fedha zilizotolewa zinajumuisha, fedha za ndani Shilingi bilioni 788.8 na fedha za nje Shilingi bilioni 175.2.

Sehemu kubwa ya fedha zilizotolewa zimeelekezwa kwenye miradi yenye vyanzo mahsusi kama ifuatavyo: Mfuko wa Barabara Shilingi bilioni 132.8; Mfuko wa Reli Shilingi bilioni 41.0; Mfuko wa REA Shilingi bilioni 53.7; Mfuko wa Maji Shilingi bilioni 24.7; na Mikopo ya Elimu ya Juu Shilingi bilioni 31.6. Maeneo mengine yaliyopata fedha ni pamoja na ugharamiaji wa elimumsingi bila ada Shilingi bilioni 41.6 na ujenzi wa hospitali za wilaya Shilingi bilioni 33.3.

## 3.3 Hatua za Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

### 3.3.1 Miradi Mikubwa ya Kielelezo

Utekelezaji halisi wa baadhi ya miradi mikubwa ya kielelezo hadi robo ya kwanza ya mwaka 2018/19 ulikuwa kama ifuatavyo:-

#### 3.3.1.1 Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha *Standard Gauge*

Kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) ujenzi wa reli umeanza na umefikia asilimia 24. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni pamoja na ujenzi wa njia, madaraja, utengenezaji wa mataruma na ujenzi wa miundombinu ya umeme. Aidha, shehena ya kwanza ya reli yenye jumla ya Tani 7,250 imewasili kutoka Japan na kazi ya kutandika kilometa 60 za reli hiyo imeanza.

Kwa kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa kazi ya kutafuta mwelekeo wa njia. Vile vile, kuendelea kufanya uthamini wa ardhi pamoja na mali. Aidha, kwa kipande cha Isaka – Rusumo (Km371), upembuzi na usanifu wa awali wa njia kwa ajili ya ujenzi wa reli hiyo unaendelea.

Zabuni kwa ajili ya kununua mabehewa, injini na mitambo itakayotumika kutoa huduma ya usafiri kwenye reli ya *Standard Gauge* ilifunguliwa tarehe 13 Julai, 2018 na tathmini ya kumpata mkandarasi huyo ipo katika hatua za mwisho. Aidha, Mawasiliano kati ya TRC na TANESCO yameendelea kufanyika ili kuunganisha

umeme kutoka gridi ya Taifa. TANESCO imeanza mchakato wa zabuni kwa ajili ya kumpata mzabuni wa kujenga mfumo wa umeme kutoka gridi ya Taifa kwenda kwenye reli hiyo.

**3.3.1.2 Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania**

Katika kipindi cha mwaka 2017/18, hatua iliyofikiwa ni kununuliwa kwa ndege moja aina ya Bombadier Q400 na moja aina ya Boeing 787 - 8 Dreamliner. Kukamilika kwa sehemu ya malipo ya ununuzi wa ndege 2 aina ya A220-300 ambazo zinatarajiwa kuwasili Novemba, 2018 na Boeing 787-8 Dreamliner moja inatarajiwa kuwasili mwaka 2020. Aidha, shughuli zinazoendelea ni pamoja na: Ukarabati wa Jengo la ofisi za Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); utafutaji wa masoko ikiwa ni pamoja na kuanzishwa kwa ofisi katika maeneo ya kimataifa ikujumuisha Bombay, Bujumbura, Guangzhou na Entebbe; kuboresha miundombinu ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na mtandao wa mawasiliano ya simu katika hangar ya uwanja wa ndege ATCL imeanza kutoa huduma za usafiri kwa miji ya Bujumbura (Burundi) na Entebbe (Uganda) mwezi Agosti 2018.

**3.3.1.3 Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji Rufiji - MW 2,100 (Rufiji hydro Power Project)**

Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu wezeshi ya kuwezesha Mkandarasi kuanza kazi kwa wakati. Hatua iliyofikiwa ni pamoja na:

(a) Ujenzi wa Njia ya Umeme wa Msongo wa kV 33 kutoka Msamvu hadi eneo la mradi: Msamvu – Pangawe (Km 14) – ujenzi umekamilika asilimia 100; Dakawa – Mpakani mwa Pori la Akiba Selous (Km 8.5) – ujezi umekamilika asilimia 100; Ndani ya Pori la Akiba la Selous – Kazi za ujenzi zinaendelea; Ujenzi wa Kituo cha Kupozea Umeme Pangawe – ujezi umekamilika asilimia 100; na Ujenzi wa Kituo cha Kupozea Umeme – umekamilika asilimia 100;

(b) Upembuzi yakinifu wa awali wa ujenzi wa njia za kusafirisha umeme (Rufiji hadi Chalinze) uliofanywa na TANESCO umekamilika na taratibu za ununuzi za kumpata Mshauri mwelekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu. Ujenzi wa njia za kusafirishia umeme kutoka Rufiji hadi Chalinze (kV 400) unatarajiwa kuanza mwezi Julai 2019. Aidha, uchambuzi wa zabuni ya kumpata Mkandarasi upo katika hatua za mwisho;

(c) Huduma ya Maji: Kufikisha maji kwenye Kambi za Ujenzi – kumekamilika asilimia 100; na Kufikisha Maji Stesheni ya Reli ya TAZARA ya Fuga – kazi inaendelea;

(d) Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi: Upimaji na uwekaji alama katika eneo la mradi – kazi zinaendelea; Ukarabati na Ujenzi wa nyumba zilizokuwa za Kambi ya RUBADA – Umekamilika kwa asilimia 55; Uthamini wa mali

zisizohamishika – kazi inaendelea; na Mpango wa Matumizi ya Ardhi katika vijiji nje ya eneo la mradi – kazi inaendelea;

(e) Barabara: Barabara ya Ubena Zomozi – Mvuha – Kisaki – Mtemere Junction (Km 178.39) – imekamilika kwa asilimia 60; na Barabara ya Kibiti - Mloka – Mtemere – Matambwe Junction – Mto Rufiji (Km 210) – imekamilika kwa asilimia 65; na

(f) Mawasiliano: Mifumo ya mawasiliano mbadala kwenye eneo la mradi imekamilika.

#### 3.3.1.4 Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia - Lindi

Serikali imeendelea na maandalizi ya mradi wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika ambapo hatua iliyofikiwa ni: kuendelea na majadiliano ya mikataba mbalimbali itakayowezesha utekelezaji wa Mradi wa LNG kati ya Serikali na Wawekezaji wa Mradi wakiongozwa na kampuni ya Shell-Tanzania na Statoil. Kazi zinazoendelea ni pamoja na kuandaa moduli ya kiuchumi ya Serikali itakayotumiwa kuongoza majadiliano kwa timu ya Serikali; kupitia moduli za kiuchumi (economic models) kutoka kwa wawekezaji (IOCs); stadi za kitaalam (technical studies) za kuandaa mpango wa kuendeleza vitalu vya baharini, zinaendelea; maandalizi ya mpango wa ushirikishaji wa wadau (stakeholders engagement plan) wa eneo la mradi; mchakato wa kumpata Mshauri Mwelekezi (Transaction Advisor); kutolewa kwa mafunzo ya mbinu za majadiliano (negotiations skills) kwa timu ya majadiliano (GNT).

#### 3.3.1.5 Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania)

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi; kukamilika kwa tathmini za kijiolojia katika eneo la Chongoleani yatakapojengwa matenki na gati la kupakia mafuta; kutiliwa kwa mkataba wa makubaliano kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda; na kuendelea na majadiliano ya mkataba wa ubia.

#### 3.3.1.6 Kanda Maalum za Kiuchumi

**(a) Eneo Maalum la Uwekezaji la Bagamoyo**

Hatua iliyofikiwa ni: ni kukamilika kwa makubaliano ya awali kati ya Serikali na wawekezaji - kampuni za CMPort State – China na State General Reserve Fund - Oman kuhusu utekelezaji wa mradi na kuendelea na majadiliano ya kina ya mikataba; na kukamilika kwa mpango kabambe wa kuendeleza eneo la hekta 175 lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Teknolojia.

**(b) Eneo Maalum la Uwekezaji la Mtwara**

Hatua ya utekelezaji iliyofikiwa ni: kuendelea na ujenzi wa miundombinu wezeshi ikiwemo ya umeme na maji.

**(c) Eneo Maalum la Uwekezaji Kigoma**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa ulipaji fidia wa hekta 691 na kupata hati miliki; kukamilika kwa hatua ya awali ya michoro kwa ajili ya kuendeleza hekta 691 na kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa awali.

**3.3.1.7 Makaa ya Mawe (Mchuchuma) na Chuma (Liganga)**

Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa taarifa ya awali ya timu ya majadiliano iliyopewa jukumu la kuchambua vivutio vilivyoombwa na mwekezaji pamoja na kuainisha maeneo ya mikataba ya mradi yanayokinzana na sheria na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa na Serikali.

**3.3.2 Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa msingi wa Uchumi wa Viwanda**

**3.3.2.1 Viwanda**

**(i) Shirika la Viwanda Vidogo - SIDO**

Uendelezaji wa viwanda vidogo: shughuli zilizofanyika ni kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya viwanda (barabara, mifumo ya maji na umeme) katika mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Manyara, Mtwara na Simiyu; ujenzi wa majengo ya viwanda (11) katika Mikoa ya Dodoma, Geita, Kagera, Katavi, Manyara, Mtwara na Simiyu na ujenzi wa ofisi za SIDO za kutolea huduma katika Mikoa mipya ya Geita na Katavi.

**(ii) Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini (CAMARTEC)**

Kazi zilizotekelezwa ni: kutengeneza zana mbalimbali na kubuni teknolojia mpya kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na ubora wa bidhaa. Zana hizo ni pamoja na mashine 64 za kupandia mbegu za pamba, kusaga karanga, kukausha mbogamboga na kukata majani; ujenzi wa mitambo 55 ya *biogas* pamoja na kutoa mafunzo na elimu ya utumiaji wa *biogas*; na kukamilika kwa tafiti tatu zinazohusiana na matumizi ya nishati mbadala ya *biogas*.

**(iii) Kiwanda cha Kuchakata Ngozi Karanga - Moshi**

Kazi zilizotekelezwa ni: ukarabati wa majengo ya kiwanda cha ngozi na bidhaa za ngozi cha Karanga-Moshi; na kupatikana kwa eneo la ujenzi wa kiwanda kipya

chenye uwezo wa kuchakata ngozi futi za mraba milioni 3.75 na kutengeneza jozi 4,000 za viatu kwa siku pamoja na bidhaa nyingine zinazotokana na ngozi. Aidha, michoro ya majengo kwa ajili ya kiwanda imekamilika.

**(iv) Mradi wa Magadi Soda – Bonde la Engaruka, Arusha**

Kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa upimaji wa ardhi na uthamini wa mali za wananchi ili kujua kiasi cha fidia kitakachohitajika; michoro ya matumizi ya ardhi hiyo ipo katika hatua za mwisho; na maandalizi ya nyaraka za zabuni kwa ajili ya kumtafuta mwekezaji yanaendelea.

**(v) Kuendeleza Kongane ya Viwanda TAMCO- Kibaha**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea kwa majadiliano na Gatsby Africa ili kuandaa Mpango Kabambe wa eneo la ekari 95 maalum kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya nguo na mavazi ujenzi wa Kiwanda cha Kutengeneza Sindano (*syringes*) unaotekelezwa na Kampuni ya El-Dawlia Limited.

**(vi) Mradi wa Kuunganisha Matrekta TAMCO - Kibaha**

Hatua iliyofikiwa ni pamoja na kuagizwa kwa sehemu (parts) zinazokamilisha matrekta 727 kati ya 2,400; kuunganishwa kwa matreka 420, majembe 95, haro 195 pamoja na baadhi ya vifaa vya ujenzi wa Kiwanda cha Kuunganisha Matrekta. Aidha ujenzi wa Kiwanda umeanza ambapo nguzo muhimu (structure) za jengo la kiwanda zimesimamishwa.

**(vii) Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo (TEMDO)**

Kazi zilizofanyika ni: kubuni mashine ya kutengeneza tofali zinazozuia upotevu wa joto (refractory bricks); majokofu makubwa; kiteketezi taka kidogo kinachobebeka kwa ajili ya zahanati na maabara za afya; mtambo wa kusindika na kusafisha mafuta ya kula na mtambo wa kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya maji na usimikaji wa mitambo wa kuzalisha umeme (kW 20) kutokana na nguvu za upepo na jua katika Kituo cha Olduvai Gorge– Ngorongoro.

3.3.2.2 Kilimo

**(a) Kilimo cha Mazao**

(i) Kupatikana kwa eneo la ekari 100 katika Kata ya Kibaigwa wilayani Kongwa, kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mazao ya nafaka;
(ii) Ujenzi wa vihenge vya kisasa na maghala mapya ya NFRA umeanza katika maeneo ya mradi ambayo ni: Songea, Makambako, Mbozi, Dodoma na Shinyanga;

(iii) Kukamilika kwa ujenzi wa ghala la kuhifadhi mazao ya wakulima wadogo katika Halmashauri ya Mbarali ambapo wakulima 950 wamenufaika; na

(iv) Katika Kuongeza Tija na Uzalishaji wa Zao la Mpunga nchini hatua iliyofikiwa ni: kuwezesha wakulima katika Halmashauri za wilaya 7 za mkoa wa Morogoro kuchagua mbegu bora za mpunga; na kufanyika kwa ziara ya mafunzo kwa wakulima 168 na wataalamu 20 katika mikoa ya Arusha na Tanga ili kujifunza na kubadilishana uzoefu wa kilimo shadidi cha mpunga na mnyororo wa thamani wa zao la mpunga; na kupatikana kwa mzabuni kwa ajili ya kusambaza pembejeo za kuendesha mashamba ya mfano ya SRI.

(b) **Mifugo**

(i) Kutekeleza Operesheni Nzagamba I iliyolenga kuongeza ufanisi katika usimamizi na udhibiti wa utoroshaji wa mifugo na mazao yake, ilikusanya Shilingi Bilioni 7.2 hivyo kuiwezesha Wizara kukusanya shilingi bilioni 19.6 ikiwa ni asilimia 20 zaidi ya lengo lililokusudiwa;

(ii) Ujenzi wa mabwawa mawili ya Olyapasei (Kiteto) na Kwamaliga (Kilindi) pamoja na lambo la Masusu katika Wilaya ya Ngorongoro;

(iii) Kuzalishwa na kusambazwa dozi 28,427,100 za chanjo ya ugonjwa wa Mdondo, dozi 882,100 za chanjo ya ugonjwa wa Kimeta, dozi 128,600 za chanjo ya ugonjwa wa Chambavu na dozi 625 za chanjo ya ugonjwa wa Kutupa Mimba;

(iv) Operesheni Nzagamba Awamu ya 2 ambayo imeanza rasmi tarehe 10 Oktoba, 2018 na itatekelezwa nchi nzima;

(v) Ukarabati wa minada ya Upili na ya Mpakani ikiwa ni pamoja na Mnada wa Kimuni ambao umezinduliwa rasmi tarehe 16 Oktoba, 2018;

(vi) Kuzinduliwa Dawati la Sekta Binafsi tarehe 1 Oktoba, 2018 likiwa na lengo la kuunganisha Serikali na Sekta Binafsi ili kuongeza uwekezaji katika sekta ya mifugo na uvuvi;

(vii) Kutayarishwa kwa Mikakati saba (7) inayolenga kuongeza maduhuli na ufanishi katika sekta ya mifugo itakayowezesha kukusanya zaidi ya sh. Bilioni 50 kwa kipindi cha 2018/2019 pamoja na kuboresha huduma mbalimbali za sekta ya mifugo;

(viii) Kuendelea kuimarishwa kwa vituo vya kanda vya uhimilishaji nchini (NAIC), ambapo mtambo wa kupoozea mbegu katika kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) kilichopo Usa River (Arusha) na mtambo wa kuzalisha kimiminika baridi cha nitrojeni katika kanda ya Mashariki (Kibaha) umefanyiwa matengenezo. NAIC pia iliimarishwa kwa

kununua madume bora ya mbegu 11 kutoka Afrika Kusini na New Zealand, kununua vifaa vya maabara, mitungi mitano ya kuhifadhi mbegu yenye ujazo wa lita 50 kila moja pamoja na mtungi wa kusafirisha kimiminika baridi cha nitrojeni wenye ujazo wa lita 2,000;

(ix) Kuhimilishwa kwa ng'ombe 508,200 pamoja na kutoa mafunzo ya unenepeshaji wa mifugo kwa walugaji 2,199 kutoka katika Halmashauri za wilaya 17 katika Mikoa ya Arusha, Manyara, Mara, Mwanza, Singida na Shinyanga;

(x) Kuimarishwa kwa miundombinu ya minada ya upili na mipakani ili kuweka mazingira mazuri ya biashara ya mifugo. Uboreshaji wa miundombinu ulihusisha: Ujenzi wa kishushio na kipakilio cha ng'ombe; kubadilisha nguzo za umeme katika mnada wa Pugu; Ujenzi wa uzio katika mnada wa Muhunze; Ujenzi wa choo mnada wa Wereweru; Kuunganisha umeme na kuchonga barabara za kuingia na kutoka (mnada wa kirumi) na kuunganisha maji katika mnada wa Kizota;

(xi) Kutengwa kwa hekta 10,378.53 kwa ajili ya maeneo ya ufugaji kwenye vijiji 13, katika Wilaya tano (5) za Makete, Kilolo, Tanganyika, Mpanda na Kalambo na kufanya jumla ya eneo lililotengwa hadi sasa kufikia hekta milioni 2.545 katika vijiji 764;

(xii) Kuzalishwa kwa marobota ya nyasi za mifugo (hay) 614,620 na 659,700 yenye wastani wa uzito wa kilo 10 kila moja kutoka kwenye mashamba ya Serikali na sekta binafsi kwa mtiririko huo;

(xiii) Kusambazwa kwa dozi 830,000 za chanjo ya sokota na dozi 1,020,000 za chanjo ya ugonjwa wa homa ya mapafu;

(xiv) Kuzalishwa na Kusambazwa kwa chanjo dozi 23,354,025 kama ifuatavyo: Brucellosis 625; Mdondo (I – 2) 22,846,500; Kimeta 426,700; na Chambavu 80,200. Vile vile, jumla ya sampuli 673 za vyakula vya mifugo zilifanyiwa uchunguzi wa viwango vya virutubisho vilivyomo na ushauri kutolewa kwa wahusika. Vilevile, Jumla ya dozi 21,600 ya chanjo ya kichaa cha mbwa zimegawanywa kwa Mamlaka za Mji Kibaha (4,800), Wilaya ya Kisarawe (4,100), Wilaya ya Dodoma (1,000), Wilaya ya Kondoa (3,000), Wilaya ya Kibaha (4,700) na Wilaya ya Babati (4,000);

(xv) Operesheni Zagamba ilianzishwa kwa lengo la kudhibiti upotevu wa mapato na usimamizi wa biashara ya mifugo na mazao yake pamoja na pembejeo za mifugo. Kiasi cha shilingi bilioni 7.2 kilikusanywa kama ushuru, tozo na faini mbalimbali katika operesheni hiyo; na

(xvi) Uratibu na usimamizi wa Sheria ya Utambuzi Usajili na Ufuatiliaji wa

Mifugo Na. 12 ulifanyika ambapo ambapo zoezi la kupiga chapa ya moto ng'ombe ilifanyika Mikoa yote ya Tanzania Bara. Jumla ya ng'ombe 17,045,944 na punda 57,797 walipigwa chapa na ng'ombe wa maziwa 58,214 walivishwa hereni. Pia wafugaji 1,462,279 walihamasishwa juu ya Sheria ya Utambuzi Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo.

(c) Uvuvi

(i) Ufugaji wa samaki kwa kutumia teknolojia ya maji kidogo yanayozunguka na kusafishwa ulifanyika kwenye miji mikubwa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya. Pia, samaki aina ya perege na kambale wameendelea kufugwa katika mabwawa ambapo mabwawa yameongezeka kufikia 24,302. Vilevile, jumla ya vifaranga vya samaki na kambamiti 15,119,757 vimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima kutoka vituo vya Serikali (243,569) vya Ruhila (176,000) na Kingolwila (67,569) na TAFIRI – Mwanza vifaranga 13,159 sato na 10,000 kambale;

(ii) Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi: kukamilika kwa taratibu za manunuzi za kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya uvuvi wa bahari kuu;

(iii) Kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania: kuendelea na taratibu za kufufua shirika ili kuongeza mchango wa Sekta ya Uvuvi katika Pato la Taifa;

(iv) Kilimo cha zao la mwani kinachofanyika katika mwambao wa bahari ya Hindi kilifanyika ambapo jumla ya tani 1,329.5 zenye thamani ya shilingi milioni 469.8 zimevunwa na kusafirishwa nje ya nchi;

(v) Shughuli za ulinzi wa rasilimali za uvuvi ziliimarishwa ambapo doria ya siku kazi 4,113 iliendeshwa katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi ambapo yalikamatwa makokoro 961, kamba za kokoro mita 800,360, nyavu za makila 27,271, nyavu za utali 2,381, mitungi ya gesi 114, baruti 4,312 detonators 358, compressors 12, kilo 302 za urea, regulators 21, vipande vya booster 943, injini ya boti 13, boti 89. Kilo 140 za kaa, kilo 9 za majongoo bahari, na makome 104;

(vi) Opereshen Sangara 2018, ilifanyika kwa ajili ya kudhibiti uvuvi na biashara haramu katika Ziwa Victoria. Viwanda vinane (8) vya kuchakata samaki vilikutwa na makosa ya kupokea na kuchakata samaki wasioruhusiwa (wachanga/wakubwa) kisheria na kutozwa faini ya shilingi milioni 285 na kupewa onyo kali. Viwanda vitatu (3) vya kutengeneza nyavu za uvuvi vilikaguliwa na kukutwa na nyavu za uvuvi zisizoruhusiwa kisheriana kutozwa faini ya shilingi milioni

690 na kupewa onyo kali na nyavu kuteketezwa. Pia, wafanyabiashara wa nyavu haramu 16 walikamatwa na kutozwa faini ya shilingi milioni 560, kupewa onyo na nyavu zao kuteketezwa; wafanyabiashara 18 wa mabondo walikaguliwa na kukutwa hawana leseni/vibali wote walitozwa faini ya shilingi milioni 690; wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi zaidi ya 1,200 walikamatwa na makosa mbalimbali na kutozwa faini na wengine kufikishwa katika vyombo vya sheria kwa hatua zaidi. Vile vile, nyavu haramu 575,152 , makokoro 11,144 , boti/mitumbwi 1,559 , magari 487 , pikipiki 176 na injini za boti 685 zilikamatwa. Pia jumla ya kilo 176,780 za samaki wachanga, kilo 183,089 za samaki aina ya Sangara waliokaushwa kwa chumvi (Kayabo) zilikamatwa na kutaifishwa. Jumla ya shilingi bilioni 9.3 zilikusanywa kutokana na faini na tozo mbalimbali. Kupitia Operesheni Sangara, 2018, uvuvi haramu katika Ziwa Victoria umepungua kwa asilimia 60 hususani matumizi ya nyavu haramu za makila;

(vii) Operesheni Jodari ilifanyika kwa madhumuni ya kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu ikiwemo uhaulishaji wa samaki (transshipment) baharini, kutoripoti takwimu sahihi za samaki waliovuliwa, uvuvaji wa samaki wasiokusudiwa na kujihusisha na biashara ya mapezi ya papa ambayo inahatarisha juhudi za uhifadhi wa rasilimali za uvuvi pamoja na uchafuzi wa mazingira na kuhakikisha uvuvi unaendana na maazimio ya kikanda ya kupambana na uvuvi haramu (IOTC Port State Measures). Meli 2 zilionekana na makossa ya kushusha tani 12.3 za samaki wasiolengwa (bycatch) kwenye bandari za hapa nchini, kutozwa na kuingiza mapato ya jumla shilling milioni 41.04 (USD 17,860). Meli hizo zilifunguliwa mashitaka. Meli ya moja ilikutwa na kosa la kufaulisha mabaharia 10 wa Kitanzania kutoka meli tano (5) na kutozwa faini. Meli 19 zenye Bendera ya China zimetozwa faini baada ya kuondoka bila kurudi bandarini kukaguliwa na kushusha samaki wasiolengwa. Aidha, Meli ya BUAH NAGA 1 iliyosajiliwa nchini Malaysia ilikamatwa katika Bahari Kuu ikiwa na mapezi ya Papa bila mili ya Papa hao kinyume cha Sheria za nchi. Meli hii ilitozwa faini na watuhumiwa kushindwa kulipa faini. Meli na Samaki vinashikiliwa na kesi ipo Mahakamani; na

(viii) Kikosi Kazi cha Kitaifa cha MATT kilifanya Operesheni dhidi ya uvuvi haramu katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani na Tanga. Lengo la operesheni ilikuwa ni kudhibiti uvuvi haramu, hususan kwa kutumia mabomu. Matokeo ya Operesheni hiyo ni kukamatwa kwa mabomu ya

milipuko 1,046, V-6 Explosives vipande 600, detonator 386 , mbolea ya Urea kilo 334 , mitungi ya gesi 77, vifaa vya kuzamia jozi 265 ,Compressors 13 na boti kumi na tano (15) zilizokuwa zikijihusisha na uvuvi wa mabomu. Kutokana na Operesheni MATT uvuvi haramu wa kutumia mabomu katika ukanda wa Bahari ya Hindi umepungua kwa asilimia 88.

### 3.3.3 Kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu

#### 3.3.3.1 Maji na Usafi wa Mazingira

(a) Kuboresha Huduma za Maji Dar es Salaam: Mradi huu unahusisha usambazaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Pwani ambapo mradi unapita. Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa asilimia 87.5 kwa upanuzi wa mtandao wa maji katika jiji la Dar es salaam ambapo maeneo ya Bagamoyo, Kibaha na Mlandizi yamesambaziwa maji. Aidha, uchimbaji wa visima 15 kati ya 20 katika eneo la Kimbiji na Mpera umekamilika na uchimbaji wa visima 5 unaendelea. Kwa ujumla utekelezaji wa shughuli ya uchimbaji wa visima umefikia asilimia 85.7;

(b) Kuimarisha Bodi za Maji za Mabonde: kujenga na kukarabati ofisi za maji za mabonde na maabara za maji katika mabonde mbalimbali ambapo hatua zilizofikiwa ni kama ifuatavyo: Ruvuma na Pwani ya Kusini (asilimia 85), Ziwa Nyasa (asilimia 50), Rufiji (asilimia 65 Mkoji na Kimani), Ziwa Rukwa (asilimia 65) na Bonde la Kanda ya Kati (asilimia 95);

(c) Kuboresha Huduma za Maji Vijijini: Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa miradi 1,595 ambapo vituo vya kuchotea maji 88,589 vimejengwa na kuhudumia wananchi 23,402,990. Aidha, miradi 492 inaendelea kutekelezwa katika Halmashauri mbalimbali; na

(d) Kuboresha Huduma za Maji Mijini: Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa asilimia 6 kwa ukarabati wa mtandao wa maji safi na maji taka katika Jiji la Arusha; kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya maji safi na usafi wa mazingira katika miji ya Sumbawanga na Lindi. Aidha, utekelezaji wa mradi huu katika mji wa Kigoma umefikia asilimia 90.

#### 3.3.3.2 Elimu

(a) Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu: Hatua iliyofikiwa ni kutolewa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu 122,623 ambapo wanafunzi 33,244 ni wa mwaka wa kwanza na 89,379 wanaendelea na masomo. Vile vile, mikopo na ruzuku imetolewa kwa wanafunzi 351 wanaoendelea na masomo nje ya nchi;

(b) Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R): Shughuli zilizofanyika ni: Kukamilika kwa ukarabati wa vyuo 7 vya ualimu vya Tandala, Nachingwea, Tarime, Patandi na Ilonga kwa asilimia 77; kukamilika kwa ujenzi wa kumbi za mihadhara wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE) kwa asilimia 90; na kukamilika kwa ujenzi wa mghahawa katika mabweni mapya ya Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kwa asilimia 95;

(c) Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA): kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kujenga uwezo kwa walimu 7,900; kukamilika kwa ukarabati wa shule kongwe 10 za sekondari za Pugu (Dar es Salaam), Mzumbe na Kilakala (Morogoro), Msalato (Dodoma), Mwenge (Singida), Tabora Wavulana na Tabora Wasichana (Tabora), Nganza (Mwanza), Ilboru (Arusha) na Same Kilimajaro;

(d) Programu ya Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu: walimu 49,000 walifundishwa katika fani ya KKK; kukamilika kwa ufuatiliaji wa mtaala mpya wa elimu ya msingi kuanzia elimu ya awali hadi darasa la nne; kukamilika na kupitishwa kwa kiunzi cha uthibiti ubora wa shule; ununuzi wa pikipiki 2,894 kwa ajili ya ukaguzi wa shule; Ununuzi wa magari 5 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uthibiti ubora wa shule; kukamilika kwa tathmini ya hali ya vyuo vya maendeleo ya wananchi 55 katika mikoa 26; na kukamilika kwa rasimu ya awali ya maudhui ya kieletroniki kwa ajili ya ufundishaji na ujifunzaji.

(e) Mradi wa Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Kampasi ya Kivukoni: Hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa hosteli ya wanafunzi yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 720 na kufungwa kwa vifaa vya kufundishia na viti visivyohamishika katika madarasa manne;

(f) Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu
Shughuli zilizotekelezwa ni:

(i) Chuo cha Ualimu Shinyanga: Kukamilika kwa ujenzi wa jengo la ghorofa mbili la nyumba za wakufunzi; ujenzi wa majengo mawili ya bweni na uzio umekamilika kwa asilimia 90; ujenzi wa majengo mawili ya madarasa, maktaba na ukumbi wa mihadhara umekamilika kwa asilimia 60;

(ii) Chuo cha Ualimu Mpuguso - Mbeya: Ujenzi wa mabweni mawili, majengo matatu ya ghorofa kwa ajili ya nyumba za wakufunzi na nyumba 1 ya kawaida umekamilika kwa asilimia 85; na ujenzi wa maktaba, maabara, ukumbi wa mihadhara, na ukumbi wa mikutano umekamilika kwa asilimia 62;

(iii) Chuo cha Ualimu Kitangali - Mtwara: Ujenzi wa nyumba 11 za

wakufunzi umekamilika kwa asilimia 68; Ujenzi wa maktaba, ukumbi wa mihadhara, majengo mawili ya mabweni na vyumba 16 vya madarasa umekamilika kwa asilimia 60; na

(iv) Chuo cha Ualimu Ndala - Tabora: Ujenzi wa nyumba tano na majengo mawili ya ghorofa kwa ajili ya wakufunzi umekamilika kwa asilimia 70.

#### 3.3.3.3 Afya

(a) Mradi wa Kuimarisha Hospitali za Rufaa

Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji ni:

(i) Hospitali ya Rufaa KCMC: kukamilika kwa ujenzi wa jengo la kutolea huduma za kliniki za Radiolojia, kinywa na meno na huduma za kisasa za uzazi; na kununuliwa kwa baadhi ya vifaa tiba ikiwemo: viti maalum vya wagonjwa, mashine maalum za *x-ray* za kinywa, na kufunguliwa kwa duka jipya la dawa la Serikali;

(ii) Hospitali ya Taifa Muhimbili: kukamilika kwa ukarabati wa jengo la upasuaji wa kina mama wajawazito; usimikaji wa *lift* mbili (2) katika majengo ya Kibasila na Mwaisela; kukamilika kwa ukarabati na usimikaji wa mfumo wa hewa katika jengo la upasuaji wa kinywa; kukamilika kwa ukarabati wa jengo kuu la upasuaji lenye vyumba 8 vya upasuaji ambapo vyumba viwili (2) ni kwa ajili ya kupandikiza figo; kukamilika kwa ukarabati wa jengo la kusafisha figo lenye jumla ya vitanda 42 vya kuchujia damu; na kuanza kwa ujenzi wa jengo maalum kwa wagonjwa wanaolipia;

(iii) Hospitali ya Rufaa Bugando: kukamilika kwa jengo la idara ya tiba ya mionzi pamoja na kufungwa kwa mashine 2 za *CT – Scan*; kununuliwa kwa mashine ya kutibu mionzi ya ndani (Brachytherapy); kununuliwa na kusimikwa kwa mashine 6 kwa ajili ya vipimo vya damu, mashine mbili (2) za vipimo vya moyo, na mshine moja ya *ultrasound*;

(iv) Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini – Mbeya: kukamilika kwa upanuzi wa jengo la uzazi na mtoto (RCH) katika kitengo cha wazazi (Meta) kwa kuongezwa vymnba vinne (4) na sehemu ya wagonjwa kusubiria huduma, na upanuzi wa eneo la mapokezi ya wagonjwa; kukamilika kwa ujenzi wa wodi za watoto; na ukarabati na upanuzi wa jengo la kutolea huduma za dharura unaendelea;

(v) Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI): kukamilika kwa ujenzi wa jengo la MOI awamu ya III; ununuzi wa vifaa tiba mbalimbali, mitambo na mashine kwa ajili ya upasuaji; ununuzi wa mashine za maabara,

mashine za radiolojia ikiwemo *CT-Scan* na MRI; na ununuzi wa mitambo ya hewa, kufua umeme, na uchomaji taka zitokanazo na huduma za afya;

(vi) Taasisi ya Saratani Ocean Road: kununuliwa na kufungwa kwa kifaa kiitwacho *"multileaf collimator"* katika mashine ya EQ80 kwa ajili ya kuboresha tiba za mionzi ya nje; kununuliwa kwa vyanzo vipya vya mionzi; kukamilika kwa ujenzi wa wodi binafsi; kukamilika kwa ukarabati wa sehemu tatu za wagonjwa kusubiria huduma; na kusimikwa kwa mashine mpya za tiba ya mionzi aina ya *"Linear Accelerator"* (LINAC) 2 na *CT Simulator"*;

(vii) Hospitali ya Rufaa ya Magonjwa ya Kifua Kikuu – Kibong'oto: kukamilika na kuzinduliwa kwa jengo la kutolea huduma kwa waathirika mahali pa kazi; na

(viii) Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe: kuendelea na ujenzi wa jengo la kuhudumia waathirika wa dawa za kulevya katika eneo la Itega.

(b) Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi: kuimarika kwa upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma katika Bohari ya Dawa (MSD) kufikia wastani wa asilimia 81 wa dawa muhimu 135; na wastani wa asilimia 92 kwa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na chanjo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

(c) Mradi wa Kudhibiti Magonjwa ya Kuambukiza: kununuliwa na kusambazwa kwa dawa za kifua kikuu na ukoma nchini; kununuliwa na kusambazwa kwa mashine za "gene-expert" 189 katika wilaya zote nchini na mashine 5 katika hospitali binafsi 5 zilizopo Dar es Salaam kwa ajili ya ugunduzi wa kifua kikuu kupitia vipimo vya vinasaba; kulunguliwa kwa vituo vipya 41 vya kutoa matibabu kwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu nchini; na kusambazwa kwa lita 236,420 za viuadudu vya kibailojia kwa ajili ya kuangamiza viluwiluwi vya mbu kwenye mazalia katika Halmashauri zote nchini.

(d) Kuimarisha Miundombinu ya Huduma za Afya: kukamilika kwa ujenzi na ukarabati wa Hospitali 10 za Wilaya, Vituo vya Afya 295 na nyumba za watumishi wa afya 306.

### 3.3.3.4 Ustawi wa Jamii

(a) Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi: uhamasishaji wanawake kujiunga na kuanzisha vikundi vya wanawake vya kiuchumi 88 vyenye jumla ya wanawake 1,517 katika Halmashauri za Wilaya ya Rombo - Kilimanjaro na Mvomero - Morogoro ambapo vimehamasishwa kujiunga na SACCOSS; na

vikundi 4,365 vyenye wanawake wajasiriamali 39,449 katika Halmashauri 130 ndani kupatiwa mikopo ya shilingi bilioni 7.3 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake;

(b) Programu ya Uhai na Maendeleo ya Mtoto: Hatua iliyofikiwa ni uelimishaji wa jamii na watoto kuhusu madhara ya mimba na ndoa za utotoni katika Mkoa wa Shinyanga ambapo wanafunzi 1,405 na walimu 283 walielimishwa; waendesha bodaboda 93 katika mkoa wa Mara (63), na Dodoma (30) kupewa elimu kuhusu haki na kutambua utu wa mtoto wa kike kwa lengo la kumlinda dhidi ya mimba za utotoni; kujengewa uwezo kwa maafisa upelelezi wa mikoa ya kipolisi 33, Polisi Makao Makuu ya Jeshi la Polisi (50) na Waratibu 417 wa Dawati la Jinsia na Watoto katika Jeshi la Polisi katika kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto; na

(c) Programu ya Uwezeshaji wa Huduma za Ustawi wa Jamii: Hatua iliyofikiwa ni wajumbe 300 wa timu za ulinzi na usalama wa mtoto katika halmashauri 15 kujengewa uwezo kuhusu ulinzi na usalama wa mtoto.

### 3.3.3.5 Utawala Bora na Huduma Bora kwa Wananchi

(a) Miradi ya Mfuko wa Bunge: kuanza kwa kazi za awali kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya makazi ya Naibu Spika eneo la Kilimani - Dodoma na nyumba ya Katibu wa Bunge – Dodoma na utekelezaji wa mradi wa Bunge Mtandao umefikia asilimia 15;

(b) Mradi wa Mfuko wa Mahakama: Kukamilisha ujenzi wa Mahakama za wilaya za Bagamoyo, Mkuranga na Kigamboni na Mahakama za Mwanzo za Kawe, (DSM), Robanda (Serengeti), Mvomero (Morogoro), Iguguno (Singida) na Bereko (Kondoa), kukamilika kwa nyumba mbili za Majaji pamoja na ukarabati wa nyumba moja katika mkoa wa Mtwara na kuendelea na ujenzi wa Mahakama ya wilaya 16 Mahakama za Hakimu Mkazi za Mikoa 5 (Geita, Njombe, Katavi, Lindi na Simiyu) na Mahakam Kuu za Kigoma na Mara. Pia kuanza maandalizi ya ujenzi wa majengo ya Makao Makuu ya Mahakama ya Tanzania mjini Dodoma;

(c) Vitambulisho vya Taifa: hatua iliyofikiwa ni kusajiliwa kwa watu 19,563,091 hadi Agosti 2018 ukilinganinisha na watu 18,681,059 mwezi Juni 2018 katika mikoa mbalimbali Tanzania Bara na Zanzibar; kukamilika kuunganishwa kwa wilaya 117 na mtandao wa mawasiliano; na kuunganishwa kwa taasisi 45 za umma na binafsi na mfumo wa Vitambulisho vya Taifa (Interface).

### 3.3.3.6 Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu

(a) Mfuko wa Maendeleo ya Vijana: Hatua iliyofikiwa ni kutolewa kwa mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.74 kwa jumla ya

vikundi vya vijana 523 kutoka katika Halmashauri 128; kuanza kutumika kwa Mwongozo wa Uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, unaosisitiza uanzishaji wa SACCOSS; kukamilika kwa ukaguzi wa ufuatiliaji wa fedha za Mfuko ambapo Halmashauri za Wilaya 19 zimerejesha shilingi milioni 235.

(b) Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi: Hatua iliyofikiwa ni kutoa mafunzo kwa vijana 10,858 katika fani mbalimbali kupitia mafunzo ya uanagenzi ambapo vijana 6,455 wamepatiwa mafunzo hayo katika fani za ushonaji wa nguo, useremala, uashi, terazo, uchongaji wa vipuri, ufundi magari, ufundi umeme, ufundi bomba, uchomeleaji, kutengeneza viatu vya ngozi na TEHAMA; vijana 3,989 walipatiwa mafunzo katika fani mbalimbali ili kurasimisha Ujuzi uliopatikana Nje ya Mfumo Rasmi; na mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi ambapo vijana 414 waliunganishwa na waajiri ili kuweza kupata ujuzi wa kuajirika ama kujiajiri wanapohitimu masomo yao.

#### 3.3.3.7 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

(a) Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Habari Tanzania (TBC): Hatua iliyofikiwa ni: kuanza kwa usanifu wa Jengo la Utangazaji Jijini Dodoma unaohusisha pia majengo mbalimbali zikiwemo nyumba za wafanyakazi; na kukamilika kwa hatua za awali za uanzishaji wa Chaneli ya Televisheni ya masuala ya Utalii ambapo vifaa kwa ajili ya ujenzi wa studio vitafungwa Novemba, 2018.

#### 3.3.3.8 Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

Hatua iliyofikiwa katika uhifadhi endelevu wa bonde la Ziwa nyasa ni kukamilika kwa uandaaji wa vitalu vya miche ya miti na uanzishwaji wa mashamba darasa katika Wilaya za Ludewa, Kyela na Mbinga.

### 3.3.4 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji

#### 3.3.4.1 Miundombinu

(a) **Barabara**

(i) Barabara ya Sumbawanga – Matai - Kasanga Port (Km 112) – utekelezaji umefikia asilimia 80;
(ii) Barabara ya Bulamba – Kisorya (Km 51) – utekelezaji umefikia asilimia 55;
(iii) Barabara ya Urambo - Kaliua (Km 28) – ujenzi umefikia asilimia 5;
(iv) Barabara ya Loliondo (Wasso) – Sale Junction (Km 49) – ujenzi umefikia asilimia 15;
(v) Barabara ya Mpemba – Isongole (Km 50.3) – ujenzi umfikia asilimia 10;
(vi) Barabara ya Sanya Juu – Alerai (Km 32.2) – imefikia asilimia 70;

(vii) Barabara ya Maswa – Bariadi (Km 49.7) – imefikia asilimia 15;

(viii) Barabara ya Kikusya – Ipinda – Matema (Km 34.6) – imefikia asilimia 78;

(ix) Barabara ya Lusitu – Mawengi (Km 50) – imefikia asilimia 10;

(x) Barabara ya Njombe – Moronga – Makete (Km 107.4) – imefikia asilimia 15;

(xi) Barabara ya Mtwara – Mnivata (Km 50) – imefikia asilimia 30;

(xii) Ujenzi wa barabara ya Morogoro sehemu ya Ubungo – Kibaha kwa njia sita unaendelea;

(xiii) Barabara ya Chunya – Makongolosi (Km 43) – imefikia asilimia 11;

(xiv) Barabara ya Makutano - Natta - Mugumu/Loliondo - Mto wa Mbu (km 185): kuendelea na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Makutano - Natta (km 50) ambapo utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 65.08;

(xv) Barabara ya Manyoni - Itigi – Tabora (km 259.7): kulipa sehemu ya madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa ujenzi wa sehemu za Manyoni – Itigi – Tabora;

(xvi) Tabora – Nyahua – Chaya: sehemu ya Tabora – Nyahua (km 85) imekamilika na Nyahua – Chaya (km 85.4) imefikia asilimia 17.60;

(xvii) Barabara ya Kidahwe - Kasulu – Kibondo - Nyakanazi (km 413): kuendelea na ujenzi kwa sehemu za Kidahwe – Kasulu (km 63) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 72; kuanza ujenzi sehemu ya Nduta – Kibondo – Kabingo (km 61.84) na barabara ya kupitia Kibondo mjini;

(xviii) Barabara ya Tabora – Koga – Mpanda: sehemu ya Tabora - Usesula (km 30) utekelezaji imekamilika, Usesula – Komanga (Km 115.5) imefikia asilimia 11.8, Komanga – Kasinde (Km 112.8) imefikia asilimia 10.0 na Kasinde – Mpanda (km 107.7) imefikia asilimia 10.0;

(xix) Barabara ya Mbinga – Mbamba Bay (Km 66) imefikia asilimia 6.0;

(xx) Barabara ya Morogoro: sehemu ya Ubungo - Kibaha kazi ya upanuzi barabara kwa njia sita unaendelea;

(xxi) Barabara ya Usagara - Geita - Buzirayombo – Kyamyorwa (Km 230): kulipa sehemu ya malipo ya Makandarasi kwa sehemu ya Uyovu - Bwanga (km 43), kuendelea na ujenzi wa barabara ya Bwanga - Biharamulo (km 67) ambapo ujenzi umefikia asilimia 80, kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Geita - Bulyanhulu Jct (km 58.3) na Bulyanhulu Jct - Kahama (km 61.7);

(xxii) Barabara za Kupunguza Msongamano jijini Dar es Salaam (km 169.66): kukamilika kwa barabara za Kimara - Kilungule – External (km 9),

Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi - Banana (km 14) sehemu ya Kifuru – Malambamawili - Msigani (km 4), Tegeta – Kibaoni - Wazo Hill – Goba - Mbezi (Morogoro road) sehemu ya Mbezi Mwisho – Goba (km 7), Tangi Bovu - Goba (km 9), Kimara Baruti – Msewe - Changanyikeni (km 2.6), Kibamba – Kisopwa – Kwembe - Makondeko (km 14.6 6) sehemu ya Kibamba –Mloganzila (km 4), Ardhi – Makongo - Goba (km 9) sehemu ya Goba - Makongo; na kuendelea na ujenzi wa barabara za Kimara – Kilungule - External (km 9), sehemu ya ya Kimara – Kilungule - Majichumvi (km 6); Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana (km 14), sehemu Msigani (km 2) na Tegeta Kibaoni - Wazo Hill – Goba (km 13), sehemu ya Madale - Goba (km 5);

(xxiii) Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (km 42.9): maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka awamu ya pili, ya tatu na nne yanaendelea; na

(xxiv) Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyover) jijini Dar es Salaam: kukamilika kwa *Mfugale flyover* (TAZARA) na kuanza kutumika. Aidha, ujenzi wa *Interchange* ya Ubungo unaendelea.

(b) Madaraja

Hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa madaraja ni kama ifuatavyo:

(i) Mara (Mara) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 81.3;
(ii) Sibiti (Singida) asilimia 79.8;
(iii) Daraja la Magara (Manyara) – imefikia asilimia 9;
(iv) Lukuledi (Lindi) asilimia 70;
(v) Ruhuhu (Ruvuma) asilimia 65;
(vi) Mlalakuwa (Dar es Salaam) asilimia 64;
(vii) Momba (Songwe) asilimia 7.5;
(viii) Daraja la Selander (Dar es Salaam) mkataba ya ujenzi imesainiwa; na
(ix) Wami (Pwani), mikataba ya ujenzi imesainiwa.

(c) Vivuko

(i) Ununuzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu: kuendelea na ujenzi wa meli mpya katika ziwa Victoria, Nyasa na Tanganyika; na
(ii) kuendelea na ukarabati wa meli za MV Victoria, MV Butiama, MV Liemba, MV Umoja, MV Serengeti na MV Songea.

(d) Viwanja vya Ndege

(i) Ujenzi wa jengo jipya la abiria (Terminal III) katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere: kuendelea na ujenzi wa jengo jipya

la abiria (Terminal III) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 78;

(ii) Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro: kukamilika kwa ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, ujenzi wa barabara ya kiungio, usimikaji wa taa za kuongozea ndege na ukarabati wa maegesho ya magari; na kukamilika kwa upanuzi wa jengo la abiria;

(iii) Kiwanja cha Ndege Mwanza: kuendelea na upanuzi wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la mizigo, uzio wa kiwanja pamoja na maegesho ya ndege za mizigo, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, kusimika taa za kuongozea ndege na ujenzi wa mfumo wa kuondoa maji ya mvua kiwanjani ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70; na

(iv) Kiwanja cha Ndege Msalato (Dodoma) – kuanza maandalizi ya ujenzi.

(e) **Nishati**

(i) Ujenzi wa Mradi wa *Kinyerezi I Extension* – MW 185: kukamilika kwa ujenzi wa misingi ya mitambo pamoja na ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kV220 (Kinyerezi I hadi Kinyerezi II);

(ii) Mradi wa kufua Umeme unaotokana na nguvu ya maji Rusumo MW 80: kukamilika kwa ujenzi wa kambi ya kudumu ya wafanyakazi; na kuendelea na ujenzi wa bwawa la kuhifadhi maji na miundombinu ya barabara;

(iii) Mradi kufua umeme wa kwa kutumia nguvumaji Ruhudji MW 358; kuendelea na majadiliano ili kuwezesha upatikanaji wa fedha za kutekeleza mradi;

(iv) Mradi wa kufua Umeme unaotokana na nguvu ya maji Malagarasi – MW 45: kuendelea kwa kazi ya kudurusu upembuzi yakinifu wa mradi;

(v) Mradi wa njia kusafirisha umeme wa Msongo wa kV 220 Makambako – Songea: hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa mradi; na

(vi) Miradi ya Kusambaza Umeme Vijijini kupitia REA (Awamu ya III): Kuunganishwa umeme kwa vijiji 557.

(f) **Bandari**

(i) Uendelezaji wa Bandari ya Dar es Salaam: kazi ya ujenzi imeanza ambapo uwekaji nguzo za msingi za Magati umekamilika katika Gati Na. 1; Ujenzi wa Gati la Ro-Ro unaendelea na upo katika hatua ya ujenzi wa sakafu ngumu chini ya maji. Utekelezaji wa mradi umekamilika kwa asilimia 35;

(ii) Kuboresha Miundombinu ya Bandari ya Tanga: Ukarabati wa

maegesho ya meli na sehemu ya kupakulia shehena na ukarabati wa miundombinu ya barabara kuelekea lango Na. 2 umekamilika kwa asilimia 76; na

(iii) Upanuzi wa Bandari ya Mtwara: ujenzi wa gati la mita 300 la kuhudumia shehena mchanganyiko umefikia asilimia 30.

### 3.3.4.2 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

Kuendelea na ukarabati na ujenzi wa majengo ya ofisi za balozi na makazi ya watumishi katika balozi za Kampala (Uganda), Kinshasa (DRC) na Brussels (Ubelgiji). Aidha, ukarabati wa majengo ya taaluma na maktaba ya Chuo cha Diplomasia (Dar es Salaam) unaendelea. Vile vile, uboreshaji wa mfumo wa udahili wa wanafunzi kwa njia ya kielektroniki unaendelea.

### 3.3.4.3 Uhamasishaji wa Sekta Binafsi

Serikali imeendelea na jitihada kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza kwenye sekta muhimu zitakazokuza uchumi kwa haraka, pamoja na kuwasaidia wajasiriamali wadogo na wakati kuibua fursa za uwekezaji kwa lengo la kukuza biashara zao na kuongeza kipato. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ziliandaa makongamano ya biashara na uwekezaji kwa kushirikisha nchi za Vietnam, India, China, Korea, Ufaransa, Israel, Hispania na uholanzi.

Aidha, Serikali imeandaa Mwongozo kwa Balozi za Tanzania Nje ya Nchi ili kuvutia mitaji, uwekezaji na kutafuta masoko na pia imeongeza miundombinu ya majengo ya mitaa na mabanda ya viwanda kwa ajili ya wajasiriamali. Vilevile, Elimu ya ujasiriamali na utoaji wa mitaji kupitia NEDF imetolewa. Hata hivyo, Wizara imeandaa Mwongozo wa Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kusambaza kwa utekelezaji. Kutokana na juhudi hizo na nyinginezo jumla ya viwanda ("cumulative") 3,306 hadi kufikia Machi, 2018 vimeanzishwa

### 3.3.4.4 Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Kwa upande wa ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo, Serikali imeendelea kuweka mikakati ya kuimarisha ushiriki wa sekta hiyo kwa uwekezaji wa moja kwa moja au kwa utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Mikakati hiyo ni pamoja na kuandaa Mwongozo wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (Blueprint for Regulatory Reforms to Improve Business Environment). Vile vile, Serikali imeendelea kuwekeza kwenye miundombinu wezeshi kama vile ujenzi wa barabara, nishati ya umeme na maji ili kuimarisha mazingira ya uwekezaji, na pia imeendelea kutoa vivutio vya kikodi kuvutia sekta binafsi kuwekeza katika maeneo ya kipaumbele. Aidha, Serikali

imefanyia marekebisho Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Sura 103 ili kuondoa changamoto za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia utaratibu wa PPP. Lengo la uwekezaji kupitia PPP ni kuishirikisha sekta binafsi kuwekeza kwenye miradi ya ubia hivyo kuongeza upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora, ujuzi na teknolojia mpya pamoja na ufanisi wa kutekeleza miradi. Kutokana na jitihada hizi, Serikali imefanikiwa kuanzisha na kutekeleza miradi mbali mbali ya Ubia ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na:

(a) Mradi wa Uendeshaji wa Huduma ya Usafiri jijini Dar Es Salaam Awamu ya kwanza (Dar Rapid Transit Project Phase1) ambao upo katika hatua ya uendeshaji chini ya Kampuni binafsi ya UDART; na

(b) Mradi wa uzalishaji wa Madawa Muhimu na Vifaa Tiba (Pwani, Mwanza na Mbeya) utakaotekelezwa na Bohari ya Dawa kwa kushirikiana na mbia wa sekta binafsi, ambao upo katika hatua ya uidhinishaji kwa ajili ya hatua za kumpata mbia.

(c) Miradi mingine iliyo katika hatua ya upembuzi yakinifu ni pamoja na: ujenzi wa Vyuo Kmri vya Ufundi; mradi wa Kufua umeme – Somanga Fungu MW 330; na Ujenzi wa Bandari ya Mwambani – Tanga.

### 3.3.5 Kuimarisha Usimamizi na Utekelezaji wa Mpango

#### 3.3.5.1 Ufuatiliaji wa Miradi katika Mwaka 2017/18

Katika mwaka 2017/18, Wizara ya Fedha na Mipango ilifuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Miradi inayofuatiliwa ni ile inayogharamiwa kwa fedha za Serikali na ile inayotekelezwa na Sekta Binafsi. Miradi 43 ilifuatiliwa katika sekta za Maji, Uchukuzi, Viwanda, Afya, Kilimo, na Elimu katika mikoa ya Pwani, Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Dodoma, Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe, Ruvuma, Mtwara, Mwanza, Dar es Salaam, Shinyanga na Lindi. Orodha ya miradi iliyofuatiliwa imeainishwa katika Kiambatisho II.

#### 3.3.5.2 Changamoto Zilizobainishwa katika Utekelezaji wa Miradi Iliyofuatiliwa

(a) Uwezo wa makandarasi wanaopewa zabuni za ujenzi katika miradi iliyofuatiliwa kutokuwa na uwezo wa kutekeleza miradi hiyo kwa wakati uliopangwa kwenye mkataba;

(b) Uhaba wa watumishi katika baadhi ya miradi iliyokamilika unaathiri ufanisi katika uendeshaji wa miradi husika;

(c) Uchakavu wa miundombinu na mitambo katika baadhi ya miradi imesababisha miradi kuzalisha chini ya kiwango kinachotakiwa; na

(d) Kukosekana kwa umeme wa uhakika katika baadhi ya viwanda

kumesababisha viwanda kupata hasara na kushindwa kupanua uwekezaji.

**3.3.5.3 Changamoto za Utekelezaji wa Mpango na Hatua Zilizochukuliwa**

Kwa ujumla, utekelezaji wa bajeti ya maendeleo una changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa wakati; maandalizi ya baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati ili kuruhusu hatua za utekelezaji kwa kuzingatia mpango kazi wa utekelezaji; na mwenendo wa kupungua kwa upatikanaji wa misaada na mikopo nafuu. Katika kukabiliana changamoto hizo, Serikali imechukua hatua zifuatazo:

(a) Kuimarisha mifumo na taasisi zinazokusanya mapato ili kudhibiti ukwepaji kodi na uvujaji wa mapato;

(b) Kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara na uwekezaji wa Sekta Binafsi; na

(c) Kutoa mafunzo ya uandaaji wa miradi ya maendeleo kwa wataalam wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Taasisi za Serikali.

# SURA YA NNE

## MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2019/20

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inaainisha maeneo ya kipaumbele yatakayozingatiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2019/20 iliyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 na Mkakati wa Utekelezaji.

### 4.2 Misingi na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

#### 4.2.1 Msingi ya Mpango kwa Mwaka 2019/20

Misingi mikuu ya uandaaji wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 ni kama ifuatavyo:

(a) Kuendelea kuimarishwa na kudumishwa kwa amani, usalama, utulivu na umoja wa ndani na nchi jirani;

(b) Kuimarika kwa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya kiuchumi na kijamii kama vile Pato la Taifa;

(c) Kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani;

(d) Utulivu wa bei nchini na katika soko la kimataifa;

(e) Kuendelea kuimarika na kutengamaa kwa uchumi wa dunia;

(f) Kuendelea kuwa na utulivu wa bei za bidhaa za petroli katika soko la dunia; na

(g) Hali ya hewa nzuri ndani ya nchi na katika nchi jirani.

#### 4.2.2 Shabaha za Ukuaji wa Uchumi

Shabaha za ukuaji wa uchumi katika mwaka 2019/20 na muda wa kati (2019/20 – 2021/22) ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.3 mwaka 2019 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 7.2 mwaka 2018 na kuongezeka kwa wastani wa asilimia 7.6 katika kipindi cha muda wa kati;

(b) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 5.0 katika kipindi cha muda wa kati;

(c) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.7 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20 kutoka matarajio ya asilimia 12.5 mwaka 2018/19 na wastani wa asilimia 12.9 katika kipindi cha muda wa kati;

(d) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 21.1 ya Pato la Taifa mwaka 2019/20 na kufikia wastani wa asilimia 20.2 katika kipindi cha muda wa kati;

(e) Kupunguza nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kutoka matarajio ya asilimia 2.9 mwaka 2018/19 hadi wastani wa asilimia 1.1 katika kipindi cha muda wa kati; na

(f) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi 4.5 katika kipindi cha muda wa kati.

### 4.3 Miradi Mikubwa ya Kielelezo na Itakayopewa Msukumo wa Kipekee

Ili kufikia malengo na shabaha tarajiwa kwa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2019/20, msukumo wa kipekee unaelekezwa katika kutekeleza miradi ya kielelezo, hususan, ifuatayo:

#### 4.3.1 Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Maji Rufiji - MW 2,100

Kuongeza uwezo wa kufua umeme, ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bwawa na mitambo ya kuzalisha umeme ambapo maandalizi ya ujenzi yalianza Januari 2018 na unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 36. Lengo la Mpango wa pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa eneo la umeme ni kufikia uzalishaji wa MW 5000 ifikapo 2020. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha ongezeko la MW 2,100 kutokana na chanzo cha maji ambacho ni nafuu zaidi na hivyo kusaidia kupunguza wastani wa gharama za uzalishaji kutokana na vyanzo vingine. Kwa kipindi cha mwaka 2019/20, kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

(a) Ujenzi wa miundombinu wezeshi ya mradi ikiwemo ujenzi wa kambi na ofisi za wafanyakazi; na

(b) Ujenzi wa bwawa na njia kuu za kupitisha maji.

#### 4.3.2 Kuendeleza ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge*

Katika kipindi cha 2019/20 kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

(a) Kuendelea na ujenzi wa reli ya Dar es Salaam – Morogoro (km 300) na kuanza ujenzi kwa kipande cha Morogoro – Makutopora (km 422);

(b) Kutafuta mwekezaji wa kipande cha Isaka – Rusumo;

(c) Kukamilisha taratibu za kutwaa ardhi kwa ajili ya njia ya reli Morogoro hadi Dodoma na maeneo mengine;

(d) Kukamilisha usanifu wa kimazingira na jamii katika eneo litakalopitiwa na mradi; na

(e) Kuimarisha uwezo wa Shirika la Reli ili liweze kusimamia na kuendesha mradi

kwa ufanisi.

**4.3.3 Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania**

Lengo la Mradi ni kuboresha uendeshaji wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL). Katika mwaka 2019/20, shughuli zitakazofanyika ni:

(a) Kukamilisha malipo ya ununuzi wa ndege aina ya Boeing 787 Dreamliner;
(b) Ununuzi wa ndege moja aina ya Airbus (A220 – 300);
(c) Kugharamia uendeshaji wa awali wa Boeing 787 Dreamliner ya pili;
(d) Kuimarisha uwezo wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji katika kutoa mafunzo ya masuala ya usafiri wa anga; na
(e) Kuanzisha Kitengo cha Kuhudumia Ndege Uwanjani (ground handling unit).

**4.3.4 Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania)**

Lengo la mradi huu ni kujenga bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania. Katika mwaka 2019/20, shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na:

(a) Uundaji wa kampuni ya mradi; na
(b) Majadiliano kati ya kampuni na benki kwa ajili ya upatikanaji wa fedha.

**4.3.5 Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia - Lindi**

Katika mwaka 2019/20, shughuli zitakazotekelezwa ni:

(a) Kukamilisha usanifu wa awali na kuanza usanifu wa kina wa kihandisi;
(b) Kukamilisha mikataba muhimu ya mradi; na
(c) Majadiliano na benki kwa ajili ya upatikanaji wa fedha za kugharamia mradi.

**4.3.6 Kiwanda cha Kufua Chuma cha Liganga**

Lengo la mradi ni kujenga mgodi wa kufua chuma na kiwanda cha kuzalisha bidhaa za chuma. Katika mwaka 2019/20, shughuli zitakazotekelezwa ni:

(a) Kukamilisha ulipaji wa fidia;
(b) Kukamilisha uchambuzi wa mikataba ya Mradi kwa kuzingatia marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2017;
(c) kuanza ujenzi wa mgodi;
(d) kufanya uthamini wa mali za wananchi watakaopisha ujenzi wa njia ya umeme kutoka Mchuchuma – Liganga; na
(e) Kuanza maandalizi ya ujenzi wa kiwanda cha chuma.

**4.3.7 Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi**

Mradi unalenga kurahisisha upatikanaji wa maeneo ya uzalishaji na uendeshaji biashara, ambapo kwa mwaka 2019/20 vipaumbele vimewekwa katika kuharakisha

utekelezaji wa kanda zilizoainishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kanda hizo ni:-

**4.3.7.1 Eneo Maalum la Uwekezaji Bagamoyo**

Lengo la mradi ni kujenga bandari ya kisasa na kuanzisha eneo maalum la viwanda. Katika mwaka 2019/20, shughuli zitakazotekelezwa ni:

(a) Kupata hati miliki ya eneo;
(b) Kujenga miundombinu wezeshi; na
(c) Kuanza ujenzi wa kituo cha teknolojia.

**4.3.7.2 Eneo Maalum ya Uwekezaji Kigoma**

Lengo la mradi ni kuanzisha eneo maalum la uwekezaji Kigoma lenye bandari huru, mitaa ya viwanda, kongane za utalii na kituo cha biashara na huduma. Katika mwaka 2019/20, shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kutafuta mwekezaji atakayeshirikiana na Serikali kwa utaratibu wa ubia.

**4.3.7.3 Eneo Maalum la Uwekezaji Mtwara**

Lengo la mradi ni kujenga bandari huru na ujenzi wa viwanda vinavyotumia gesi asilia. Katika mwaka 2019/20, shughuli zitakazotekelezwa ni:

(a) Kufanya upembuzi yakinifu na kuandaa *master plan;*
(b) Ujenzi wa miundombinu wezeshi; na
(c) Kutangaza eneo la bandari kwa wawekezaji (wabia) wa maendeleo na kusimika mitambo.

**4.3.7.4 Eneo maalum la Uwekezaji Ruvuma**

Lengo la mradi ni ujenzi wa viwanda vikubwa vitakavyotumia malighafi za gesi na chuma. Katika mwaka 2019/20, shughuli zitakazotekelezwa ni:

(a) Kukamilisha ulipaji wa fidia;
(b) Kupata hatimiliki ya eneo;
(c) Kufanya upembuzi yakinifu;
(d) Kuandaa mpango kabambe; na
(e) Kufanya tathmini ya athari za kimazingira.

**4.3.8 Kusomesha kwa Wingi Wataalam kwenye Fani na Ujuzi Adimu.**

Eneo hili lina lenga maendeleo ya ujuzi maalum kwa ajili ya uchumi wa viwanda na maendeleo ya watu, na kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu. Ujenzi wa uchumi wa viwanda utahitaji nguvukazi yenye fani na ujuzi adimu na bobezi kuendana na mahitaji ya viwanda hususan katika nyanja za mafuta na gesi asilia, uhandisi, urubani, udaktari bingwa, na ufundi. Kwa mwaka 2019/20, hatua

zitakazochukuliwa ni kama ifuatavyo:

**4.3.8.1 Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili**
Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya majengo ya utawala, kumbi za mihadhara na semina, maabara, maktaba, na hosteli za wanafunzi ili kuongeza udahili wa wanafunzi wa udaktari.

**4.3.8.2 Hospitali ya Rufaa ya Benjamin Mkapa – Dodoma**
Kuendelea na ujenzi wa kumbi za mihadhara na; ujenzi wa maktaba (medical library); ujenzi wa hosteli na Cafeteria, na kusimika miundombinu ya umeme na maji.

**4.3.8.3 Kugharamia mafunzo katika fani adimu na maalum**
Kuendelea kugharamia mafunzo ndani na nje ya nchi katika fani za mafuta na gesi asilia, TEHAMA, urubani, uongezaji thamani wa madini, kilimo cha biashara, uhandisi na udaktari bingwa.

**4.3.8.4 Utafiti na Maendeleo (Research and Development)**
Katika mwaka 2019/20 shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na:
(a) Kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika ugharamiaji wa shughuli za tafiti;
(b) Kuimarisha Taasisi za Tafiti za Viwanda na uanzishaji wa maabara za kupima ubora; na
(c) Kuimarisha uratibu wa shughuli za tafiti nchini.

## 4.4 Viwanda vya Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

**4.4.1 Viwanda**
Katika mwaka 2019/20 Serikali inatarajia:
(a) Kuimarisha shughuli za Shirika la Viwanda Vidogo – SIDO;
(b) Kuendeleza maeneo maalum ya uwekezaji ikiwemo Manyoni na Dodoma;
(c) Kuendelea kujenga viwanda vinavyotumia malighafi za ndani ya nchi ikiwemo kilimo, madini na gesi asilia;
(d) Kuhakikisha upatikanaji wa mitaji ya kuendeleza viwanda kupitia Benki ya Rasilimali na Benki ya Maendeleo Kilimo na mifuko ya wajasiriamali wadogo;
(e) Kuimarisha uanzishwaji na uendelezaji wa kongane za viwanda vinavyotumia malighafi za mazao ya kilimo na shughuli nyingine za kiuchumi ikijumuisha maeneo ya viwanda (Industrial parks) na maeneo ya

Teknolojia (Technological Parks);

(f) Kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 1996 – 2020 (Sustainable Industrial Development Policy - SIDP) na kuandaa Mkakati wa Utekelezaji.

(g) Kuendelea na utekelezaji wa mikakati mikuu ya kuendeleza sekta za alizeti, ngozi na bidhaa za ngozi, pamba mpaka mavazi, na viwanda vya dawa;

(h) Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Viwanda Mama na Miradi ya Kimkakati;

(i) Kufanya tathmini ya hali halisi ya uzalishaji viwandani pamoja na mahitaji ya bidhaa za viwanda ikiwemo sekta ya sukari, mafuta ya kula; vifaa vya ujenzi, chuma, mbao na bidhaa za mbao, ngozi na bidhaa za ngozi, nguo na mavazi na usindikaji vyakula (mchele, unga, mbaazi na vyakula vingine); na

(j) Kuimarisha na kuzitumia taasisi za umma katika kuleta mageuzi ya viwanda nchini. Taasisi hizo ni pamoja na: NDC, STAMICO, TPDC, CARMATEC, TEMDO, COSTECH, na Nyumbu na Mzinga.

### 4.4.2 Kilimo

#### 4.4.2.1 Kilimo cha Mazao

Kwa mwaka 2019/20 Mpango wa maendeleo utajielekeza kwenye kilimo kitakacho hakikisha usalama wa chakula ili kukabiliana na tatizo la njaa na upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda. Maeneo yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na:

(a) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji;

(b) Ujenzi na ukarabati wa maghala, masoko na miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo;

(c) Kuweka mfumo endelevu wa upatikanaji wa mbegu na pembejeo nchini;

(d) Kufanya utafiti wa kilimo na mifugo na kuzalisha teknolojia (katika mahindi, mhogo, ngano, michikichi, ufuta, alizeti, pamba, na mpunga);

(e) Kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za mazao na mifugo na kuzisambaza kwa wakulima;

(f) Kuboresha maarifa na ujuzi kwa watafiti kupitia mafunzo mbalimbali ili kuwawezesha kufanya utafiti kwa weledi na tija;

(g) Kuanzisha utaratibu wa bima ya mazao;

(h) Kuimarisha huduma za upimaji wa matabaka na ubora wa ardhi kuendana na mahitaji ya mazao ya kilimo kimaeneo;

(i) Kuimarisha vituo vya utafiti kwa kujenga miundombinu ikiwemo ofisi ya makao makuu ya TARI na kuongeza vitendea kazi vya utafiti; na

(j) Kutoa huduma za ushauri kuhusu utafiti, mafunzo na usambazaji taarifa za kilimo na sayansi shirikishi.

#### 4.4.2.2 Mifugo

Kwa kuzingatia idadi na tija ya mifugo iliyopo, katika mwaka 2019/20, msukumo utawekwa katika maeneo yafuatayo:

(a) Kuimarisha vituo vya uhamilishaji kitaifa na kikanda;
(b) Kuimarisha huduma za utafiti, ugani na mafunzo kwa maafisa ugani;
(c) Kuboresha miundombinu ya uzalishaji mifugo, machinjio na masoko;
(d) Kuongeza thamani bidhaa za mifugo;
(e) Kuimarisha sekta ya nyama na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa na kuhamasisha unywaji wa maziwa;
(f) Kuimarisha usimamizi wa ardhi kwa kutenga maeneo ya malisho; na
(g) Kuimarisha tiba na udhibiti wa magonjwa ya mifugo.

#### 4.4.2.3 Uvuvi

Katika sekta ndogo ya uvuvi, msukumo utawekwa kwenye:

(a) Kuimarisha shughuli za utafiti, huduma za ugani na mafunzo ya uvuvi;
(b) Kuendelea na uhamasishaji wa ufugaji wa samaki;
(c) Kuimarisha, kusimamia na kuendeleza rasilimali za uvuvi pamoja na kutunza mazingira;
(d) Kusimamia na kuhamasisha uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu na viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi; na
(e) Kuanza maandalizi ya ujenzi wa bandari ya uvuvi.

#### 4.4.2.4 Misitu na Nyuki

Katika mwaka 2019/20 maeneo yatakayopewa kipaumbele ni:

(a) Kuendelea kuimarisha taasisi zinazohusika na usimamizi na uendelezaji wa misitu na ufugaji nyuki;
(b) Kusimamia na kuendeleza rasilimali za misitu na ufugaji nyuki; na
(c) Kuimarisha usimamizi wa ardhi oevu na bioanuai.

### 4.4.3 Wanyamapori

Katika mwaka 2019/20 msukumo utaelekezwa kwenye maeneo yafuatayo:

(a) Kuimarisha Mamlaka za Usimamizi wa wanyamapori;
(b) Kutokomeza uwindaji haramu wa wanyamapori na kuendeleza hifadhi;
(c) Kuboresha miundombinu kwenye hifadhi za wanyama; na
(d) Kuendelea kutatua migogoro kati ya wananchi na Mamlaka za Usimamizi hifadhi za wanyamapori.

### 4.4.4 Madini

Maeneo ya vipaumbele kwa sekta ya madini kwa mwaka 2019/20 ni kama

ifuatavyo:

(a) Kuboresha sera na sheria za usimamizi wa madini;

(b) Kuweka miundombinu itakayohakikisha shughuli za uongezaji thamani madini nchini ili kuongeza mapato na ajira;

(c) Kuimarisha mfumo wa ukaguzi na uthamini wa shughuli za migodi ili kuwepo na usimamizi endelevu wa rasilimali za madini;

(d) Kuimarisha uzalishaji na biashara ya madini nchini; na

(e) Kuweka mazingira wezeshi ya kusaidia shughuli za wachimbaji wadogo nchini.

#### 4.4.5 Utalii, Biashara na Masoko

(a) Ujenzi, ukarabati na kutangaza maeneo ya vivutio vya utalii nchini, hususan ukanda wa kusini.

(b) Kuongeza wigo wa utalii kwa kuboresha na kutangaza vivutio kama Malikale, Historia, na utalii wa kiutamaduni;

(c) Kuongeza ujuzi katika taaluma ya uhifadhi wa vivutio vya utalii, kuhifadhi na kukuza utamaduni;

(d) Kukuza na kuendeleza bidhaa za kitalii;

(e) Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato yatokanayo na utalii.

(f) Kuendelea kuboresha mazingira ili kuiwezesha Tanzania kunufaika na fursa za kibiashara zilizopo kwenye masoko ya kimataifa;

(g) Kuboresha mifumo ya mitandao;

(h) Kutangaza bidhaa za Tanzania kupitia makongamano mbalimbali;

(i) Kuboresha mazingira ya kufanya biashara kwa kupitia na kupunguza vikwazo visivyo vya kikodi;

(j) Ujenzi na ukarabati wa masoko ya mipakani;

(k) Kuendelea kuboresha masoko kwa bidhaa za Tanzania; na

(l) Kuwawezesha wajasiriamali wa Tanzania kutangaza bidhaa za ndani.

### 4.5 Kufungamanisha Uchumi na Maendeleo ya Watu

Lengo la eneo hili ni kuweka mazingira mazuri ya ustawi kwa wananchi hususan wa vijijini kuwa na afya bora, elimu na ujuzi, ustawi wa jamii na kupunguza umasikini. Mapendekezo ya vipaumbele katika eneo hili ni;

#### 4.5.1 Elimu na Ujuzi

##### 4.5.1.1 Elimu ya awali, Msingi na Sekondari

(a) Kuandaa mfumo wa kuthibiti ubora katika sekta ya elimu;

(b) Kuboresha mazingira ya utoaji elimu katika ngazi ya shule za awali, msingi

na sekondari ikijumuisha ujenzi wa madarasa, mabweni na maabara;
(c) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya vifaa muhimu vya kujifunzia na kufundishia wanafunzi wenye mahitaji maalum;
(d) Kuendelea kuboresha mafunzo elimu ya ualimu;
(e) Kuhakikisha upatikanaji wa vifaa bora vya utafiti;
(f) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Elimumsingi bila malipo;
(g) Kuongeza ufaulu katika masomo ya hesabu, sayansi na kiingereza katika ngazi zote za elimu; na
(h) Kuendelea kutoa elimu inayozingatia mahitaji halisi ya soko la ajira.

#### 4.5.1.2 Vyuo vya Ufundi na Teknolojia
(a) Kukarabati, kujenga na kupanua miundombinu ya kufundishia na kujifunzia;
(b) Kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza;
(c) Kuongeza upatikanaji wa vitabu na vifaa vya kufundishia na kujifunza; na
(d) Kuendelea na ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi katika mikoa yenye uhaba wa vyuo hivyo.

#### 4.5.1.3 Elimu ya Juu
(a) Upanuzi na ukarabati miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya elimu ya juu;
(b) Kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wenye sifa;
(c) Kuendeleza shughuli za utafiti, sayansi, teknolojia na ubunifu;
(d) Kuendelea kuongeza upatikanaji wa vitabu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia; na
(e) Kuboresha miundombinu ya TEHAMA.

### 4.5.2 Afya na Ustawi wa Jamii

#### 4.5.2.1 Afya
(a) Kuboresha mfumo wa huduma na miundombinu ya zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, hospitali za Rufaa za Mikoa, hospitali za Rufaa za Kanda na hospitali ya Taifa;
(b) Upanuzi na ukarabati wa vyuo vya afya nchini;
(c) Kuboresha mifumo ya kinga dhidi ya magonjwa yanayoambukiza kama malaria, VVU na UKIMWI na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza;
(d) Kuimarisha programu za afya shuleni hususan kwa watoto wadogo;
(e) Kupima VVU kwa watoto chini ya Miaka 15;
(f) Kuimarisha na kuwezesha upatikanaji wa vifaa tiba katika hospitali za wilaya, mikoa, kanda na ngazi ya Taifa;

(g) Kuboresha upatikanaji wa huduma za afya za kibingwa nchini;

(h) Kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa lishe bora kwa maendeleo ya mtoto katika hatua za awali; na

(i) Kujenga hospitali za wilaya na mikoa katika mikoa na wilaya mpya nchini.

#### 4.5.2.2 Ustawi wa Jamii

(a) Kuandaa na kusimamia mfumo wa utoaji wa hifadhi ya Jamii kwa wazee;

(b) Kuandaa mfumo wa kielektroniki wa usajili katika hifadhi ya jamii;

(c) Kuimarisha taasisi za maendeleo ya jamii (CDTIs) na kuandaa wataalam wa Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii;

(d) Kuendeleza Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi;

(e) Upanuzi na ukarabati wa miundombinu katika makazi ya wazee;

(f) Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi;

(g) Kulinda haki na kuchochea maendeleo ya wanawake na watoto;

(h) Kuboresha huduma kwa maendeleo ya mtoto katika hatua za awali kwenye maeneo ya kazi, biashara na jamii.

### 4.5.3 Maji na Usafi wa Mazingira

(a) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji safi na salama kwa wote vijijini na mijini;

(b) Kuimarisha shughuli za Mfuko wa Maji;

(c) Kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji nchini;

  (i) Kukamilisha ujenzi wa mabwawa makubwa (Farkwa, Kidunda na Ndembera); na

  (ii) Kuendeleza usimamizi wa mazingira na vyanzo vya maji.

(d) Ukarabati, ujenzi na kuimarisha taarifa za ubora wa maabara za maji;

(e) Kuhamasisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika miradi ya maji;

(f) Kuendeleza utekelezaji wa miradi mikubwa ya maji ya Kitaifa; na

(g) Kuimarisha mifumo ya uchunguzi wa Usafi wa Mazingira kwa wote.

### 4.5.4 Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu

Katika kuhakikisha ajira zinatolewa kwa makundi ya vijana na walemavu, Mpango utazingatia mambo yafuatayo:-

(a) Kuendeleza Ujuzi na Stadi za Kazi katika kilimo, viwanda, miundombinu, biashara, utalii, usafirishaji, TEHAMA na madini;

(b) Kuimarisha mfuko wa maendeleo ya vijana ili kuongeza upatikanaji wa mitaji; na

(c) Kurasimisha stadi na ujuzi unaotoka nje ya mfumo rasmi wa mafunzo.

**4.5.5 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**

(a) Kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya michezo;

(b) Kuimarisha usikivu wa vyombo vya habari vya Serikali mijini na vijijini;

(c) Kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia wawekezaji kuwekeza katika vyombo vya habari vya Umma;

(d) Uibuaji na uendelezaji wa vipaji katika tasnia ya Sanaa;

(e) Kuibua na kuendeleza vipaji vya michezo mbalimbali;

(f) Kutekeleza mradi wa kuhifadhi kumbukumbu za urithi wa ukombozi wa bara la Afrika; na

(g) Kuboresha tasnia ya Sanaa na Ubunifu.

**4.5.6 Utawala Bora na Huduma Bora kwa Wananchi**

(a) Kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi iliyo chini ya mifuko ya Bunge na Mahakama;

(b) Kuendelea kusajili matukio muhimu ya binadamu, hususan vizazi na vifo, ili kuendelea kuboresha na kuimarisha daftari la watu nchini;

(c) Kuendeleza utambuzi, usajili wa watu pamoja na uzalishaji wa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi (wazawa), wageni wakazi pamoja na wakimbizi waishio nchini kihalali;

(d) Kuendelea na ukamilishaji wa azma ya kuhamishia shughuli za Serikali Kuu kwenda Dodoma;

(e) Kuendelea kuboresha ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mashtaka ya Taifa na Wakili Mkuu wa Serikali ili huduma muhimu za kisheria ziweze kuwafikia wananchi katika ngazi ya halmashauri;

(f) Kuendelea na ujenzi wa nyumba za viongozi wakuu wa kitaifa wastaafu kwa mujibu wa sheria;

(g) Ununuzi wa ardhi maeneo ya kimkakati kwa matumizi ya Idara ya Uhamiaji;

(h) Kuendelea na ujenzi wa vituo vipya vya polisi na magereza ili kukidhi mahitaji ya huduma za utoaji haki zinazoendana na ongezeko la watu nchini;

(i) Ununuzi wa Magari saba ya Kuzima moto pamoja na Vifaa vya Kuzima moto na maokoazi;

(j) Kuanza maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika mwaka 2022; na

(k) Kuanza maandalizi ya Uchaguzi Mkuu mwaka 2020 na uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019.

**4.5.7 Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi**

(a) Kuimarisha usimamizi wa miradi ya mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi;

(b) Kuimarisha Mfuko wa Mazingira nchini; na
(c) Kuimarisha taasisi zinazohusika na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabia ya nchi.

## 4.6 Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara na Uwekezaji

Katika mwaka 2019/20, mapendekezo yatajikita katika kuendeleza na kushnamia ujenzi na ukarabati wa miundombinu wezeshi iliyoanza na inayoendelea kutekelezwa katika mwaka 2018/19. Aidha, Serikali itatekeleza maelekezo yaliyotolewa katika Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kulanya Biashara Nchini wa 2010 ikiwa ni pamoja na kusimamia mapendekezo yaliyo kwenye *Blueprint*. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

### 4.6.1 Miundombinu

#### 4.6.1.1 Reli

(a) Kuimarisha uwezo wa kusafirisha abiria na mizigo kwa Shirika la Reli Tanzania;
(b) Kuendelea kuboresha miundombinu ya TAZARA ili iweze kutoa huduma kwa ufanisi;
(c) Kuendelea kuboresha mfumo wa kitaasisi wa TAZARA;
(d) Kuendelea na ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya reli za TRC;
(e) Kuendelea na maandalizi ya awali kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usafiri wa treni za abiria Dar es Salaam; na
(f) Kuboresha mfumo na huduma zinazotolewa katika treni za abiria Dar es Salaam.

#### 4.6.1.2 Barabara

(a) Kukarabati na kujenga barabara zinazounganisha Tanzania na nchi jirani;
(b) Kujenga na kukarabati barabara za mikoa kwa kiwango cha lami;
(c) Kujenga na kukarabati barabara zenye kufungua fursa za kiuchumi;
(d) Kuendelea kujenga barabara za kupunguza msongamano katika jiji la Dar es salaam, Dodoma, Mbeya, Arusha na Mwanza;
(e) Kuendelea na ujenzi wa barabara za juu katika jiji la Dar es salaam; na
(f) Kuimarisha mtandao wa barabara za vijijini na mijini.

#### 4.6.1.3 Bandari

(a) Ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya bandari nchini;
(b) Kuendelea na ununuzi wa vifaa vya kuhudumia shehena katika bandari na maziwa makuu; na
(c) Kuendelea na ujenzi wa bandari kavu.

**4.6.1.4 Nishati**

(a) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya uzalishaji umeme;

(b) Kujenga na kukarabati miundombinu ya usafirishaji na usambazaji umeme mijini na vijijini;

(c) Kuimarisha miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia; na

(d) Kuendeleza shughuli za utafiti katika sekta ya mafuta na gesi asilia.

**4.6.1.5 Madaraja**

Kuendelea kujenga na kukarabati madaraja makubwa.

**4.6.1.6 Usafiri wa Majini**

(a) **Meli**

(i) Kuendelea na ujenzi wa meli za abiria na mizigo katika maziwa makuu; na

(ii) Kuendelea kukarabati meli zilizosimama na zinazoendelea kutoa huduma katika maziwa makuu.

(b) **Vivuko**

(i) Ununuzi wa vivuko vipya katika bahari na maziwa;

(ii) Ujenzi na ukarabati wa maegesho ya vivuko;

(iii) Ununuzi wa vifaa vya usalama na uokozi katika bahari na maziwa makuu; na

(iv) Ukarabati wa vivuko vilivyopo katika bahari na maziwa.

**4.6.1.7 Usafiri wa anga**

(a) Kuimarisha viwanja vya ndege na miundombinu yake;

(b) Kujenga viwanja vipya vitano;

(c) Kuhimarisha usalama wa shughuli za usafiri wa anga;

(d) Kuendelea kuboresha kiwanja cha ndege cha Dar es Salaam kuwa kitovu cha usafiri wa anga; na

(e) Kuimarisha miundombinu ya huduma za utabiri wa hali ya hewa.

**4.6.1.8 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano**

(a) Kuanza maandalizi ya awali kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kutengeneza vifaa vya TEHAMA vilivyoisha muda wake (Electronic parts Recycling Plant);

(b) Kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano;

(c) Kuendelea na utekelezaji wa Anuani za Makazi; na

(d) Kuboresha kituo cha kutengeneza progamu za TEHAMA.

**4.6.2 Ardhi na Maeneo ya Uwekezaji na Biashara**

(a) Kuimarisha milki za ardhi ikiwemo urasimishaji makazi mijini, kujenga Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi pamoja na kujenga ofisi za ardhi za mikoa;

(b) Kuimarisha mipaka ya kimataifa na nchi jirani na upimaji wa ardhi;

(c) Kuwezesha upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi ikiwemo Mfuko wa Fidia wa Ardhi;

(d) Kufanya tafiti kuhusu mbinu na teknolojia rahisi za uzalishaji wa vifaa vya ujenzi wa nyumba bora kwa gharama nafuu na kusambaza matokeo ya tafiti hizo kwa umma;

(e) Kutekeleza mradi wa kuwezesha umilikishaji ardhi kwa wananchi;

(f) Kuimarisha miundombinu ya vyuo vya ardhi;

(g) Kuandaa ramani za msingi ili kurahisisha upimaji wa ardhi; na

(h) Kujenga Kituo cha kupokea picha anga.

**4.6.3 Huduma za Fedha**

(a) Kuendelea kukuza mitaji na kuimarisha huduma zitolewazo na benki za maendeleo;

(b) Kuongeza idadi ya mikopo ili kunufaisha wananchi wengi zaidi na kukuza uwekezaji;

(c) Kuboresha mifumo ya kukusanya marejesho;

(d) Kutafuta mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kukuza mitaji ya benki;

(e) Kufanya maboresho ya kimfumo ili kuwezesha wateja kupata mikopo na kurejesha mikopo kwa kutumia teknolojia ya kimtandao;

(f) Kuboresha mazingira ya kutolea huduma kwa kuongeza matawi na vituo vya kutolea huduma; na

(g) Kuendelea kutoa mikopo ya muda wa kati na muda mrefu.

**4.6.4 Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa**

(a) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo na ofisi za Balozi za Tanzania;

(b) Kuendelea kuboresha Miundombinu ya Chuo cha Diplomasia;

(c) Kuendelea kuvutia fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali; na

(d) Kuendelea kuratibu makubaliano ya kikanda, kimataifa na kufungua balozi mpya na Konseli Kuu (Colsulates General).

**4.6.5 Ushiriki wa Sekta binafsi, Mashirika na Taasisi za Umma katika Mpango**

**(a) Sekta Binafsi**

Serikali na Taasisi zake inatambua jukumu la msingi la Sekta Binafsi katika

utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Hivyo, Serikali itaendelea na uhamasishaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Mashirika ya Umma katika kuongeza uwekezaji hususan kwenye maeneo ya kipaumbele kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2019/20 kama vile:-

(i) Kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo katika kuwekeza kwenye viwanda na maeneo mengine ya kimkakati ikiwemo chuma, madini na makaa ya mawe; na

(ii) Kushirikiana na wadau wa maendeleo kuwekeza katika miundombinu wezeshi hususan kwenye maeneo ya bandari, barabara, mawasiliano, reli na viwanja vya ndege, nishati na uendelezaji miji.

**(b) Uwekezaji wa Sekta binafsi**

Sekta binafsi inatarajia kuongeza uwekezaji ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo hususan katika maeneo ya kipaumbele kama yalivyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 ikiwemo:Viwanda vya nguo, madawa, bidhaa za ngozi, usindikaji wa vyakula, mafuta, ujenzi wa miundombinu wezeshi, huduma za jamii, huduma za fedha, huduma za utalii; na kuanzisha na kuendeleza maeneo ya viwanda na maeneo ya Teknolojia.

**(c) Mchango wa Serikali katika kuimarisha Ushiriki wa Sekta binafsi**

Kwa lengo la kujenga mazingira wezeshi ili kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi, Serikali imepanga kutekeleza mikakati mbalimbali katika mwaka 2019/20 ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha mazingira wezeshi na vivutio vya kipekee ili kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika maeneo ya kipaumbele, hususan viwanda;

(ii) Kuimarisha majadiliano kati ya serikali, sekta binafsi na wawekezaji;

(iii) Kuendelea na maboresho hususan ya kimfumo na kimiundo kwa mashirika na ofisi za umma katika kutatua changamoto zinazoikumba sekta binafsi;

(iv) Kurahisisha zoezi la upatikanaji wa ardhi yenye hatimiliki kwa wawekezaji; na

(v) Kushirikisha Sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya huduma za kijamii kwa njia ya PPP.

**(d) Miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kupitia mfumo wa ubia kati ya sekta za Umma na Binafsi. Maboresho hayo yamepelekea kuwekwa kwa mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi ikiwa ni pamoja na kuandaliwa kwa Sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Lengo la miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ni kuhakikisha kupatikana kwa huduma bora, ujuzi na teknolojia mpya katika kuendesha miradi na ufanisi katika utekelezaji wa miradi. Aidha, kupitia mfumo huu mchango wa Serikali katika kugharamia miradi yenye mwelekeo wa kibiashara unapungua hivyo kuweza kuelekezwa katika shuguli nyingine muhimu za kijamii.

Miradi ya PPP inayopendekezwa kutekelezwa ni pamoja na: Mradi wa Kusambaza Gesi Asilia nchini katika mikoa ya Dar es Salaam, Lindi na Mtwara; Mradi wa Kujenga Hosteli ya wanafunzi katika Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE); mradi wa ujenzi wa vyuo kumi vya Ufundi; mradi wa kujenga Taasisi ya Taifa ya Saratani; ujenzi wa Reli ya Mtwara - Mbababay kupitia Mchuchuma na Liganga; Ujenzi wa reli ya Tanga – Arusha – Musoma; na ujenzi wa bandari ya Mwambani Tanga; mradi wa Kufua umeme – Somanga Fungu; mradi wa Uendeshaji wa Huduma ya Usafiri jijini Dar Es Salaam Awamu ya kwanza; na mradi wa ujenzi wa viwanda vya uzalishaji wa dawa muhimu na vifaa tiba katika mikoa ya Pwani, Mbeya na Mwanza.

### 4.7 Usimamizi wa Utekelezaji wa Mpango

Mapendekezo ya Mpango yanalenga kuimarisha utekelezaji wa Mpango na miradi ya maendeleo. Miongoni mwa masuala yanayopewa msukumo ni pamoja na upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu na kwa riba nafuu, kuimarisha ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa matumizi, kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwa kuzingatia Mkakati wa Utekelezaji. Maeneo mengine ni yale ya kujenga mazingira wezeshi hususan, kulinda umoja wa kitaifa, ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo na ulinzi wa rasilimali za Taifa.

# SURA YA TANO

## UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA 2019/20

### 5.1 Utangulizi

Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 unazingatia makadirio ya awali yaliyofanyika kwa kuangalia vigezo vifuatavyo: mwenendo wa viashiria vya uchumi; ukusanyaji wa mapato ya Serikali; upatikanaji wa michango ya Washirika wa Maendeleo; na uwekezaji wa sekta binafsi. Vile vile, yamezingatia Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21. Mpango huu unatarajiwa kugharamiwa na sekta ya umma na binafsi kupitia uwekezaji wa moja kwa moja au kwa njia ya ubia.

### 5.2 Gharama za Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2019/20

Katika Mwaka 2019/20, Serikali inakadiria kutumia Shilingi bilioni 12,384.4, ikilinganishwa na shilingi bilioni 12,007.3 zilizotengwa kwa mwaka 2018/19. Kiasi hiki kilichotengwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ni sawa na asilimia 37.0 ya bajeti yote. Kati ya kiasi hicho, Shilingi bilioni 9,555.7, sawa na asilimia 77.2 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 2,828.7 ni fedha za nje. Kiwango hiki kimekidhi wigo wa kutenga fedha za maendeleo kati ya asilimia 30 hadi 40 ya bajeti yote kama ilivyoelekezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21.

Serikali itatumia mikakati mbalimbali ili kufanikisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ugharamiaji wa Mpango. Mikakati hiyo inajumuisha: kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara ili kuvutia uwekezaji zaidi wa sekta binafsi katika maeneo ya kipaumbele; kuendelea kurasimisha sekta isiyo rasmi ili kukuza mchango wake katika uchumi; kuendelea kuimarisha usimamizi wa kodi na utoaji wa elimu ya mlipakodi ili kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani; na kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kupitia utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo (Development Corporation Framework - DCF).

### 5.3 Vyanzo vya Mapato kwa Mwaka 2019/20

Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, ambao unaainisha hatua za kimkakati za kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuongeza makusanyo katika vyanzo vilivyopo. Hatua hizo zitajumuisha: kuimarisa ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuongeza mchango wa Washirika wa Maendeleo katika Mpango; kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia wawekezaji wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; kuongeza

mchango wa mashirika na taasisi za umma; na kutumia vyanzo bunifu vya kuongeza mapato kama vile soko la fedha na mitaji.

Katika kuongeza makusanyo kutoka katika vyanzo vya ndani, Serikali itaendelea kutumia soko la ndani kukusanya mitaji ya uwekezaji bila kuathiri maendeleo ya sekta binafsi nchini kwa kupunguza mikopo ya ndani ya muda mfupi na kuongeza mikopo ya muda mrefo na nafuu katika riba na kutoa nafasi ya utekelezaji wa miradi mikubwa.

Kwa upande wa vyanzo vya nje vya mapato, Serikali itaendelea kuimarisha Ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kwa kuhimiza utekelezaji wa ahadi za mikopo na misaada; kukopa kwenye vyanzo vya masharti nafuu; na kupunguza mikopo ya kibiashara.

# SURA YA SITA

# UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

## 6.1 Utangulizi

Ufanisi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unahitaji mifumo imara ya ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa. Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2011/12 – 2015/16 yaliarisha changamoto mbalimbali ikiwemo udhaifu katika ufuatilaji na tathmini katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa msingi huo, Serikali iliandaa Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ambao umalenga kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Kupitia mkakati huo, mfumo wa upangaji na uwekaji wa viashiria vya utekelezaji utaimarishwa ambapo msukumo umewekwa katika kutekeleza vipaumbele vilivyopo; utoaji wa fedha kulingana na vipaumbele vilivyopo; kulinda fedha kwa ajili ya kutekeleza maeneo ya kipaumbele (ring-fencing); mifumo ya ufuatiliaji na tathmini za kisekta; na kutenga fedha kwa ajili ya shughuli za ufuatiliaji na tathmini.

## 6.2 Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21

Serikali inaendelea na taratibu za kufanya tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21 kwa kipindi cha muda wa kati. Tathmini hiyo itafanywa na Mtaalam Elekezi (Independent Evaluator) ambaye ataifanya kazi hiyo kwa uhuru. Mtaalam huyo pamoja na masuala mengine ataisaidia Serikali kutambua changamoto halisi za utekelezaji wa miradi. Matokeo ya tathmini hiyo yatatoa mapendekezo ya mabadiliko yanayohitajika ili kuhakikisha malengo ya Mpango yanafikiwa kama yalivyopangwa.

## 6.3 Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa 2019/20

Serikali itaendelea kutumia mbinu mbalimbali kwa lengo la kufikia malengo tarajiwa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mbinu hizo ni pamoja na kudhibiti, kukagua, kufanya mapitio, utafiti, usimamizi na ufuatiliaji na tathmini. Msisitizo umewekwa katika mgawanyo wa majukumu ya ufuatiliaji, uratibu, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji pamoja na upatikanaji wa taarifa za uhakika zitakazotumika kupima mafanikio kwa kutumia viashiria vya kitakwimu na visivyo vya kitakwimu. Mfumo huu utaimarisha uwezo wa uchambuzi na utoaji taarifa utakaoiwezesha Serikali kufanya maamuzi na kutoa taarifa kwa umma ili kuleta tija

na ufanisi katika utekelezaji wa Mpango.

## 6.4 Mgawanyo wa Majukumu

### 6.4.1 Wizara na Taasisi za Umma

Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyobainishwa katika mpango wa maendeleo itafanywa katika Wizara na Taasisi husika. Taarifa za utekelezaji zitaandaliwa kwa kila robo mwaka na kwa mwaka na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, miradi ya kielelezo, kimkakati na inayotekelezwa na sekta binafsi itafuatiliwa na kufanyiwa tathmini na Wizara ya Fedha na Mipango, kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi husika. Lengo la ufuatiliaji na tathmini ni kubaini changamoto zinazokabili utekelezaji wa miradi hiyo na kuzitafutia ufumbuzi.

### 6.4.2 Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo itakayotekelezwa katika ngazi za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa itaratibiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Aidha, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaelekezwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo za kipindi cha robo mwaka na mwaka Ofisi ya Rais – TAMISEMI ili ziwasilishwe Wizara ya Fedha na Mipango.

### 6.4.3 Sekta binafsi

Sekta Binafsi ni wadau muhimu katika utekelezaji wa Mpango hivyo, wanahamasishwa kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa Mpango kwa kutoa taarifa zitakazosaidia kufanya mapitio ya sera na sheria ili kuboresha mazingira ya uwekezaji.

## SURA YA SABA

## VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA KINGA

### 7.1 Utangulizi

Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 unaweza kuathiriwa na vihatarishi mbalimbali katika kufikia malengo yaliyokusudiwa. Vihatarishi vimegawanyika katika makundi mawili ambavyo ni vya ndani na nje. Vihatarishi hivyo vinaweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan katika maeneo ya ugharamiaji, muda na ufanisi katika utekelezaji wa miradi. Iwapo vihatarishi hivyo vitajitokeza, Serikali itachukua hatua madhubuti za kukabiliana na viashiria hivyo ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/20.

### 7.2 Vihatarishi vya Ndani na Mikakati ya Kukabiliana navyo

Vihatarishi vya ndani ni vile ambavyo udhibiti wake upo ndani ya uwezo wa mamlaka ya nchi. Vihatarishi hivi na mikakati ya kukabiliana navyo vimebainishwa katika Jedwali 7.1.

**Jedwali 7.1: Vihatarishi vya Ndani na Mikakati ya Kukabiliana navyo**

| NA | VIHATARISHI | MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO |
|---|---|---|
| 1. | Upungufu wa rasilimali (fedha na watu) | • Kuongeza mapato ya ndani kwa kuwianisha mapato na matumizi;<br>• Kuharakisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi;<br>• Kulinda (ringfence) fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili zigharamie shughuli zilizopangwa;<br>• Kutumia vyanzo bunifu vya mapato; na<br>• Kuendelea kuweka mikakati ya kuongeza ujuzi kwa wataalam. |
| 2. | Uharibifu wa Mazingira | • Kujenga uelewa wa wananchi juu ya utunzaji wa mazingira;<br>• kujenga uwezo wa kitaasisi katika kukabiliana na majanga; na<br>• kuendelea kushirikisha wananchi na wadau katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa miradi hususan kuhusu suala la utunzaji wa mazingira. |
| 3. | Umiliki wa ardhi na usimamizi wa migogoro | Kuhakikisha uwepo wa mipango na usimamizi wa matumizi bora ya ardhi na mipango miji inayoendana na kasi ya ukuaji wa miji na shughuli za maendeleo ili kurahisisha utoaji wa huduma za kijamii. |
| 4. | Migongano ya maslahi | Kuhakikisha kuwa wadau wote wa utekelezaji wa miradi |

| NA | VIHATARISHI | MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO |
|---|---|---|
| | | ya maendeleo wanajikita katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa. |
| 5. | Ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo | • Kuimarisha na kuendelea na majadiliano ya mara kwa mara kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika kutatua changamoto za uwekezaji;<br>• Kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya biashara, hususan katika sekta ya fedha ili kuwezesha sekta binafsi kukopa zaidi kwa ajili ya uwekezaji; na<br>• Kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP). |
| 6. | Usalama mtandaoni | Kuimarisha mfumo wa matumizi ya mitandao kwa kila taasisi kuwa na anuani yake na yenye usimamizi madhubuti. |
| 7. | Migogoro na uhalifu | Kuimarisha mfumo wa usimamiaji na utekelezaji wa sheria na taratibu ikiwemo mfumo wa utoaji haki katika ujumla wake. |

### 7.3 Vihatarishi vya Nje na Mikakati ya Kukabiliana navyo

Vihatarishi vya nje ni vile ambavyo udhibiti wake upo nje ya uwezo wa mamlaka ya nchi. Vihatarishi hivyo na Mikakati ya kukabiliana navyo vimefafanuliwa katika Jedwali 7.2.

**Jedwali 7.2: Vihatarishi vya Nje na Mikakati ya Kukabiliana navyo**

| NA | VIHATARISHI | MIKAKATI YA KUKABILIANA NAVYO |
|---|---|---|
| 1. | Mtikisiko wa kiuchumi kikanda na kimataifa | • Kuendelea na jitihada za kupunguza utegemezi kwa kuwianisha mapato na matumizi;<br>• kuongeza mapato ya ndani na kuharakisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi; na<br>• Kuongeza matumizi ya rasilimali zinazopatikana nchini kukidhi mahitaji ya Taifa. |
| 2. | Majanga asilia na mabadiliko ya tabia ya nchi | Kuimarisha mifumo ya kutambua mapema majanga na kuchukua tahadhari pamoja na kutekeleza miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi na uwezo wa kinga. |
| 3. | Siasa za kimaeneo ikiwemo vita na migogoro | Kujenga uwezo wa majadiliano na ushiriki katika kuzuia matukio ya okmayo na siasa mbaya pindi yanapotishia kutokea kimataifa na kikanda. |
| 4. | Mabadiliko ya Teknolojia | Kuhamasisha uwekezaji kutoka nje ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia duniani |
| 5. | Kubadilika kwa hitajio la bidhaa ambazo taasisi ililenga kuzalisha kwa ajili ya soko la nje | • Kufanya utafiti wa kina wa mahitaji ya soko la nje kabla ya uzalishaji;<br>• Kuzalisha bidhaa mbadala kulingana na mahitaji ya soko; |

| | | |
|---|---|---|
| | | • Kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa; na<br>• Kuchochea mahitaji ya soko la ndani. |

## Kiambatisho I: Ratiba ya Maandalizi ya Mpango 2019/20

| Shughuli | 2018 | | | | | | 2019 | | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jul | Aug | Sep | Oct | Nov | Dec | Jan. | Feb. | Mar | Apr | May | Jun | |
| Maandalizi ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 | | V | V | V | | | | | | | | | Wizara ya Fedha na Mipango |
| Kupata maoni ya wadau kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2019/20 | | | V | | | | | | | | | | Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika/ Taasisi, Wakala wa Serikali na Sekta Binafsi |
| Kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 katika hatua za maamuzi Serikalini | | | | V | | | | | | | | | Waziri wa Fedha na Mipango |
| Kuwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 | | | | | V | | | | | | | | Waziri wa Fedha na Mipango |
| Kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 | | | | | | | V | V | V | | | | Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika/ Taasisi, Wakala wa Serikali na Sekta Binafsi |
| Kupata maoni ya wadau kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 | | | | | | | V | | V | | | | Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara, Idara zinazojitegemea, Mashirika/ Taasisi, Wakala wa Serikali na Sekta Binafsi |

| Shughuli | 2018 | | | | | | 2019 | | | | | | Mhusika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jul | Aug | Sep | Oct | Nov | Dec | Jan. | Feb. | Mar | Apr | May | Jun | |
| Kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 katika Bunge Zima likikaa kama Kamati ya Mipango | | | | | | | | | | V | | | Wizara ya Fedha na Mipango |
| Kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 na Hali ya Uchumi 2018 katika Kamati ya Bajeti ya Bunge | | | | | | | | | | V | | | Waziri wa Fedha na Mipango |
| Kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2019/20 na Hali ya Uchumi 2018 katika Bunge | | | | | | | | | | | | V | Waziri wa Fedha na Mipango |
| Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka 2018/19 | | | V | | | V | | | V | | | V | Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara za Serikali |

**Kiambatisho II: Miradi Iliyofuatiliwa katika Mwaka 2017/18**

| [illegible] | [illegible] | [illegible] | [illegible] |
|---|---|---|---|
| 1. | Kiwanda cha Goodwill Ceramic LTD | Pwani | Viwanda |
| 2. | Eneo la viwanda TAMKO | Pwani | Viwanda |
| 3. | Chuo cha Mafunzo ya Mifugo | Morogoro | Elimu |
| 4. | Ujenzi wa Bwawa la Kidunda | Morogoro | Maji |
| 5. | Ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha standard gouge | Dar - Morogoro | Uchukuzi |
| 6. | Ujenzi wa jengo la Saratani katika hospitali ya rufaa ya Bugando | Mwanza | Afya |
| 7. | Ujenzi wa Meli ziwa Victoria | Mwanza | Uchukuzi |
| 8. | Ujenzi wa kivuko kipya cha Kigongo - Busisi | Mwanza | Uchukuzi |
| 9. | Upanuzi wa Mtandao wa Usafirishaji maji kutoka ziwa Victoria hadi mji wa Kishapu kupitia mji wa Manganzo, Kolandoto, na mgodi wa almasi wa Mwadui | Shinyanga | Maji |
| 10. | Ujenzi wa jengo la ghorofa kumi la chuo cha DIT | Dar es salaam | Elimu |
| 11. | Kampuni ya wakulima wa Chai Mwakaleli | Mbeya | Kilimo |
| 12. | Ujenzi wa daraja la Magufuli katika mto kilombero kwenye barabara ya Mikumi – Ifakara – Mahenge | Morogoro | Ujenzi |
| 13. | Ujenzi wa Maabara ya Maji | Mbeya | Maji |
| 14. | Kituo cha utafiti TALIRI | Mbeya | Mifugo |
| 15. | Ujenzi wa Ghala la Taifa la kuhifadhi nafaka | Songwe | Kilimo |
| 16. | Ujenzi wa Jengo la Ghorofa 2 la X Ray Katika Hospitali ya Rufaa ya Nyanda za Juu Kusini | Mbeya | Afya |
| 17. | Kiwanda cha Mtanga Food Products | Iringa | Viwanda |
| 18. | Ujenzi wa hospitali ya Benjamin Mkapa | Dodoma | Afya |
| 19. | Kiwanda cha KEDA (T) CERAMICS CO. LTD (zamani Twyford) | Pwani | Viwanda |
| 20. | Skimu ya umwagiliaji Kongogo | Dodoma | Maji |
| 21. | Skimu ya umwagiliaji DAKAWA | Morogoro | Maji |
| 22. | Skimu ya umwagiliaji RUVU | Pwani | Maji |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 23. | Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) – Kihonda | Morogoro | Elimu |
| 24. | Ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi | Njombe | Elimu |
| 25. | Eneo Maalum la Uwekezaji Ruvuma | Ruvuma | Viwanda |
| 26. | Mradi wa Maji Ruvuma | Ruvuma | Maji |
| 27. | Ukarabati wa Maabara ya Maji | Ruvuma | Maji |
| 28. | Mradi wa Maji Makonde | Mtwara | Maji |
| 29. | Ujenzi wa Maabara ya Maji | Mtwara | Maji |
| 30. | Kiwanda cha Chumvi cha Magereza | Lindi | Viwanda |
| 31. | Mradi wa Usambazaji wa maji wa Handeni Trunk Main | Tanga | Maji |
| 32. | Kiwanda cha A to Z Textile Mills LTD | Arusha | Viwanda |
| 33. | Kiwanda cha Maziwa cha the Grande Demam Co. Ltd | Arusha | Viwanda |
| 34. | Ukarabati wa Chuo cha Ufundi Arusha (Arusha Technical College) | Arusha | Elimu |
| 35. | Hospitali ya Kilimanjaro Christian Medical Centre (KCMC) | Kilimanjaro | Afya |
| 36. | Kituo cha Utafiti na Mafunzo ya Kilimo KATRIN (Kilombero Agricultural Training and Research Institute) | Morogoro | Kilimo |
| 37. | Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji Msolwa | Morogoro | Kilimo |
| 38. | Mradi wa ujenzi wa Barabara ya Kidatu - Ifakara | Morogoro | Ujenzi |
| 39. | Kiwanda cha Sukari Kilombero | Morogoro | Viwanda |
| 40. | Skimu za Umwagiliaji Magonzi ikijumuisha ujenzi wa ghala na uwepo wa vifaa wezeshi (mashine) kuendesha mradi | Iringa | Kilimo |
| 41. | Kiwanda cha Maziwa ASAS | Iringa | Viwanda |
| 42. | Mamlaka ya usambazaji maji safi na Maji taka Iringa (Iringa Water Supply and Sanitation Authority – WSSA) | Iringa | Maji |
| 43. | Uwanja wa ndege Iringa | Iringa | Uchukuzi |